

RAHA YA MAHABA
**Harmonize**, Kajala wajiachia
UKURASA 20



**Bayern** Munich sasa kumkosa Gnabry
UKURASA 21

MAISHA
FEBRUARI 14, 2021 Nipashe
Baba, Mama na Mwana *Jumapili*



Ukurasa 10
Ukiendekeza ukali kwa mtoto utamuharibu



MAISHA NI NYUMBA
Kuwa mbunifu kupangilia nyumba ya nafasi ndogo



HARUSI
Ukurasa 12



14
UKURASA 9


# Nipashe JUMAPILI

Jumapili Februari 14, 2021 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • No. 0580491
www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US


# Upofu waitesa familia

• **Kila** anayezaliwa ana ulemavu huo... *Endelea ukurasa 4*



Spika wa Bunge, Job Ndugai, akiwaongoza wabunge kutoa heshima za mwisho kwa mwili wa aliyekuwa Mbunge wa Muhambwe (CCM), Injinia Atashasta Nditiye, katika viwanja vya Bunge, jijini Dodoma jana, kabla ya mwili wake kusafirishwa kwenda mkoani Kigoma kwa mazishi. **PICHA: BUNGE**

## Serikali yawajibu kina Nape kodi kwa mtutu

UKURASA 2

## SMS ya mwisho ya Nditiye kwa Spika

UKURASA 4




Scan Hapa
Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu
Google Play
App Store


MICHEZO **SIMBA SC YATETEMESHA AFRIKA** UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6

# Muswada kubana ndege zisizo na rubani wapelekwa bungeni

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

SERIKALI imewasilisha bungeni muswada wa marekebisho ya sheria mbalimbali ambapo pamoja na mambo mengine, unalenga kuzibana kurusha ndege zisizo na rubani kutokana na sababu za kiusalama.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Ofisi ya Katibu wa Bunge jana, muswada huo uliowasilishwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Prof. Adelardus Kilangi, katika Sheria ya Usafiri wa Anga, wanapendekeza kuipa Mamlaka ya Usafiri wa Anga uwezo wa kuzuia ndege zisizo na rubani kuruka bila kibali maalum.

"Pia, inapendekezwa kuipa uwezo mamlaka kuingia makubaliano ya kiutendaji na mamlaka za nchi nyingine ili kuiwezesha mamlaka kuruhusu nchi hiyo kufanya ukaguzi kwa ndege za Tanzania zinazofanya biashara na nchi hiyo au nchi nyingine inayofanya biashara na Tanzania," alisema.

Kuhusu Sheria ya Mawakili, alisema inalenga kuanzisha Kamati za Maadili za Mawakili kwa ngazi ya mkoa ili kurahisisha upatikanaji wa haki.

"Pia, kumwezesha mwananchi anayemlalamikia wakili kwa ukiukaji wa maadili kushughulikia tatizo lake katika ngazi ya mkoa bila ya uhitaji wa kusafiri kuifuata kamati ya maadili katika ngazi ya taifa," alisema.

Kwenye Sheria ya Usajili wa Vizazi na Vifo, muswada huo unapendekeza ubadilishanaji wa taarifa za usajili wa matukio muhimu baina ya taasisi moja na nyingine.

Kuhusu Sheria ya Majina ya Biashara, muswada unapendekeza majina ya biashara yanayosajiliwa yawe ni ya wale tu wanaokidhi vigezo vya kusajiliwa kwa madhumuni mahsusi.

Pia inapendekezwa kuongeza adhabu ya faini ili kuhakikisha adhabu inayotolewa na sheria inaendana na wakati na hivyo kuzuia utendaji wa makosa.

Katika Sheria ya Kampuni, muswada unapendekeza kuhakikisha watu wenye sifa ya kusajili kampuni ni wale tu wenye sifa na watapaswa kuwasilisha taarifa zao binafsi.

Pia, unapendekeza kuweka katazo au zuio la kusajili kampuni kwa watu waliowahi kutiwa hatiani au ambao taarifa zao zimetolewa na mamlaka husika kuwa mwombaji wamekuwa wakijihusisha na makosa yanayohusiana na utakatishaji fedha, ufadhili wa ugaidi, biashara ya binadamu, biashara ya dawa za kulevya au makosa mengine yanayohusiana nayo.

Inapendekezwa katika muswada huo kuruhusu watu wenye umri wa zaidi ya miaka 70 kuteuliwa kuwa wakurugenzi wa kampuni.

Kwenye Sheria ya Mahakama za Migogoro ya Ardhi, inapendekezwa kubadilisha muhula wa kushikilia nafasi kwa wenyeviti wa mabaraza ya ardhi na nyumba ya wilaya.

Muswada huo unapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Mahakama za Mahakimu ili kuwaondoa wazee washauri wa mahakama katika mahakama za mwanzo kwa kuwa mahakama hizo sasa zinasimamiwa na mahakimu wakazi wenye weledi wa sheria na hivyo kuongeza kasi ya utoaji haki kwa wakati.

"Muswada pia unapendekeza kuwaruhusu mawakili wa kujitegemea na wale wa serikali kuwawakilisha wateja wao kwenye mahakama za mwanzo hususan zinazosimamiwa na mahakimu wenye shahada," alisema.

Katika hatua nyingine, Waziri wa Katiba na Sheria Dk.Mwigulu Nchemba, amewasilisha muswada wa mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya Usajili wa Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu, unaopendekeza kumpa mkurugenzi mtendaji wa bodi mamlaka ya kufililisha makosa chini ya sheria hiyo, ili kuokoa muda na gharama zinazohusiana na uendeshaji wa mashauri mahakamani.



Waziri wa Katiba na Sheria, Mwigulu Nchemba, akihitimisha hoja na michango ya mpango wa Serikali wa miaka mitatu na mitano uliowasilishwa kwenye kikao cha pili cha mkutano wa 12 uliohitimishwa bungeni, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**.

## Maji kuwakomboa wasichana sekondari

**Na Marco Maduhu, SHINYANGA**

WANAFUNZI wa kike wanaosoma katika Shule ya Sekondari Masengwa, wilayani Shinyanga, wanatarajia kuondokana na adha ya kukatisha masomo yao kwa ujauzito kutokana na kufuata maji umbali mrefu, baada ya mradi wa maji kutoka Ziwa Victtoria kuelekezwa shuleni huko.

Eta Elisoni, mwanafunzi wa kidato cha tatu katika shule hiyo, alibainisha matarajio yao hayo juzi wakati Bodi ya Wazabuni ya Wakala wa Maji Vijijini (RUWASA) mkoani Shinyanga, ilipokagua utekelezaji wa miradi ya maji ya Ziwa Victoria katika Kijiji cha Masegwa inakopatikana shule hiyo.

Alisema katika shule hiyo, wanafunzi wa kike huwa wanaishi bwenini, lakini kikwazo kikuu cha maendeleo yao kielimu ni kufuata maji umbali wa takriban kilomita moja kutoka shuleni na kwamba huko njiani hukutana na vishawishi na kujikuta baadhi yao wakiacha masomo kwa kupewa ujauzito.

"Wasichana ambao tuanaishi hosteli hapa shuleni huwa tunakabiliwa na changamoto ya ukosefu wa maji, na tunapofuata maji kijiji jirani cha Mwamatongo, hukumbana na vishawishi vya kutongozwa kila siku na baadhi yetu hupata ujauzito na kuacha masomo," aliwasilisha kilio chao.

Mkuu wa Shule hiyo, Salu Mlyambate, alisema tatizo la ukosefu wa maji shuleni hapo limekuwa kikwazo kitaaluma kwa wanafunzi wa kike ambao wanaishi bwenini kwa kuwa hupoteza muda wa masomo kufuata maji na wengine kuingia kwenye uhusiano ya kimapenzi na wanakijiji.

Meneja Wakala wa Maji Vijijini (Ruwasa) mkoani Shinyanga, Julieth Payovela, alisema mradi huo wa maji katika Kijiji cha Masengwa, unatarajiwa kukamilika Februari 28, mwaka huu na kusambaza maji kijijini huko zikiwamo taasisi za serikali, ukigharimu Sh. milioni 234.

# Waziri awajibu kina Nape ukusanyaji kodi kwa mtutu

**Na Godfrey Mushi, DODOMA**

SERIKALI imetetea uamuzi wake wa kutumia vikosi kazi 'task force' katika kukusanya kodi kwa wafanyabiashara na walipa kodi wakubwa wanaokwepa kodi, ikifafanua kuwa kabla ya kutumia kikosi, hutumwa kwanza timu maalum kwenda kukagua ikiwahusisha maofisa wa Mamlaka ya Mapato (TRA) na wataalamu wengine.

Waziri wa Katiba na Sheria, Dk. Mwigulu Nchemba, amesema serikali hufanya hivyo panapotokea watu wanafanya njama za kukwepa kodi, ndipo Kamishna Mkuu wa TRA, hutumia sheria inayomruhusu kutengeneza kikosi kazi kwa mujibu wa Sura ya 348 ya Sheria ya Utawala wa Kodi.

Dk. Mwigulu alitoa ufafanuzi huo jana bungeni alipokuwa anajibu hoja za wabunge waliohoji uhalali wa matumizi ya kikosi kazi kukusanya kodi.

Hoja hiyo iliibuliwa bungeni Februari 9, mwaka huu na Mbunge wa Mtama (CCM), Nape Nnauye, akidai ukusanyaji wa kodi kupitia vikosi kazi unaua biashara na kushauri kazi hiyo ifanywe na wenye taaluma chini ya TRA.

Pia, Mbunge wa Geita Mjini (CCM), Costantine Kanyasu, alisisitiza ni lazima Wizara ya Fedha na Mipango iwasikilize wananchi kwa sababu inawezekana hawana taarifa sahihi, hivyo biashara zinakufa.

Katika hotuba ya kuhitimisha mjadala huo jana aliyoitoa kwa niaba ya Waziri na Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, Waziri Mwingulu alisema:

"Tuna kipindi tumekipita ambacho kulipa kodi, elimu ya mlipakodi, uhiari na uzalendo ilikuwa jambo kubwa na gumu sana kwa watu watu walio wengi, hasahasa wafanyabiashara wakubwa.

"Nendeni mkafuatilie 'hansad' (taarifa) za Bunge lile lililopita, fuatilieni hansad muone kilio kikubwa kilikuwa wapi.

"Kilio kikubwa kilikuwa walipakodi hasa wakubwa, hawalipi kodi ipasavyo. Walipakodi waliokuwa wanabeba nchi, ni watumishi wa umma kwa kiwango kikubwa, na walipakodi wadogo wadogo na baadhi yao walipakodi wakubwa waliokuwa waaminifu. Kwa hiyo kuna kiwango kikubwa sana cha ukwepaji wa kodi.

"Sasa, hivi jambo linaloanza kujitokeza la kwamba task force ndio zinakusanya na TRA imeacha majukumu yake, ninaomba nilihakikishie Bunge lako tukufu kwamba TRA bado wanaendelea kukusanya mapato wao wenyewe, na pale ambapo inatokea task force inakusanya, kunakuwapo hatua zinazofuatwa.

"Kunakuwapo na taarifa kwamba kwa mlipakodi huyu kuna viashiria vya kutokulipa kodi ipasavyo. Baada ya hapo, kunatumwa timu ya kwenda kukagua, timu ya kawaida ambayo ni TRA na wataalamu wao huenda kukagua. Wakishakagua wanaambizana, wanaelekezana kwa mujibu wa sheria."

Waziri huyo alisema kuwa kabla ya kikosi kazi kwenda kufanya kazi yake, TRA kwa kutumia sheria zake, hujadiliana na mlipakodi katika yale makadirio, wanakubaliana na wakati mwingine wanatiliana saini.

HABARI KITAIFA

# Nyumba ya Nyerere yapata maji kwa mara ya kwanza

**Na Beatrice Shayo**

NYUMBA aliyokuwa anaishi Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere, miaka 58 iliyopita katika eneo la Shule ya Sekondari Pugu jijini Dar es Salaam, jana ilipata maji kwa mara ya kwanza baada ya huduma hiyo kufikishwa kwenye eneo hilo.

Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, jana alizindua njia ya maji katika nyumba hiyo baada ya kufanya ziara ya ukaguzi wa maendeleo ya mradi wa maji Kisarawe-Pugu-Gongo la Mboto ambao unatekelezwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira (DAWASA) kwa gharama ya Sh. bilioni 6.9.

Alisema Mwalimu Nyerere alikuwa akiishi kwa miaka 58 iliyopita na kipindi chote hapakuwa na maji hadi jana alipozindua huduma hiyo.

"Kama serikali tungefurahi sana kama leo mzee wetu angekuwapo kwenye nyumba hiyo, tukamzindulia maji akayaona yanatoka.

Ni ukweli usiojificha kuwa tumechelewa sana, lakini tumefanya, ni fahari yetu kwamba nyumba hii ya kihistoria tumekuja kufungua njia ya maji kwa Dar es Salaam Kusini kutoka hapa kwenye nyumba ya kihistoria.

"Sisi inatupa faraja kuwa maagizo ya Baba wa Taifa, maagizo ya mwasisi wetu tumeyafanyia kazi na leo tumefanya ushahidi na Watanzania wanaona na ni imani yetu na hili tunalolifanya, naye anaendelea kupumzika salama huko aliko," alisema.

Samia alisema watafanya ziara za mara kwa mara kufuatilia kama maagizo wanayoyatoa yanafanyiwa kazi.

Alisema watakapokwenda kuzindua wiki ya maji, watanzunguka Tanzania yote kwenye miradi ya maji kwa lengo la kuangalia kazi walizowapa kama zimetekelezwa.

"Ziara nilivyofanya ya Bagamoyo, ilikuwa na maneno maneno kidogo. Kwanini Makamu wa Rais ameruka Mkoa wa Dar es Salaam wakati hatuna maji, lakini DAWASA walijipanga, hivyo tuanzie huko na baadaye nije Dar es Salaam kwa sababu huko ndiko kuna chanzo kikubwa cha maji," alisema.

Alisema takwimu za Mganga Mkuu wa Wilaya ya Ilala zinaonyesha maeneo ya Ukonga, Segerea na maeneo yao kuna maradhi makubwa yatokanayo na ukosefu wa majisafi na salama, hivyo kupatikana kwa maji hayo kunakwenda kupunguza wimbi la maradhi hayo kwa wananchi.

Alisema DAWASA wamefanya kazi nzuri katika mradi huo kwa gharama ambazo zinakubalika na mwelekeo wa serikali ni kupunguza gharama za utekekezaji wa miradi ya maji.

Samia alisema mamlaka hiyo imeahidi kuwa watakapotoka madarakani mwaka 2025, Dar es Salaam itakuwa imepata maji kwa asilimia 100 na hakuna ambaye atakosa maji jijini humo.

Samia aliwataka wananchi kuacha mchezo wa kuharibu miundombinu ya maji kwa kuwa serikali inatumia gharama kubwa katika kuwawekea maji, hivyo ni vizuri wakawa wazalendo katika kuilinda.

Mwenyekiti wa Bodi ya DAWASA, Jenerali mstaafu Davis Mwamunyange, alisema tangu mamlaka hiyo ilipoanzishwa, matokeo yake ni mazuri na wamejipanga upya kutekeleza miradi mbalimbali mikubwa na midogo.

"Siyo maji yanatoka mara moja kwa wiki, tunataka tuhakikishe huduma ya maji inapatikana kila wakati kwa saa 24, huo ndiyo mkakati wetu," alisema.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa DAWASA, Cyprian Luhemeja, alisema mamlaka hiyo imejipanga kutekeleza miradi yake kwa kutumia fedha zao kwa kuwa walipewa maelekezo na wizara kutumia asilimia 35 ya mapato yao katika miradi.

Alisema mradi wa Ukonga ni mkombozi kwa wananchi kwa sababu walikuwa wanapata shida ya maji, akitamba kuwa kata zote zitapata maji na ifikapo Desemba mwaka huu, maji yatapatikana kwa asilimia 100 kwa mkoa mzima.

Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Abubakar Kunenge, alisema Sh. trilioni moja zimewekezwa kwenye miradi ya maji kwa mkoa huo na tatizo la maji litakuwa ni historia.

Mbunge wa Ukonga, Jerry Slaa, alisema kazi kubwa waliyofanya ni kuleta maendeleo kwa fedha zao wenyewe katika kutekeleza miradi badala ya kuwategemea wafadhili.



Nyumba aliyokuwa akiishi Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere, wakati alipokuwa akifundisha Shule ya Pugu Sekondari kuanzia mwaka 1952 hadi mwaka 1955, iliyopo Pugu Juu, Mkoa wa Dar es Salaam. **PICHA: OMR**

# Kiswahili sasa rasmi lugha ya sheria

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

BUNGE limepitisha Muswada wa Marekebisho ya Sheria mbalimbali wa Mwaka 2021, ambao pamoja na mambo mengine, unapendekeza Kiswahili kutumika kama lugha ya sheria na mahakama.

Akisoma maudhui ya muswada huo jana bungeni, Waziri wa Katiba na Sheria, Dk. Mwigulu Nchemba, alisema unapendekeza kufanyiwa marekebisho katika sheria tatu ambazo ni Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sheria ya Mahakama za Migogoro ya Ardhi na Sheria ya Mahakama za Mahakimu.

Alisema sehemu ya pili ya muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Tafsiri ya Sheria ili kufanya marekebisho katika kifungu cha 84 kwa kuondoa matumizi ya Kiingereza kama lugha ya sheria na mahakama na badala yake kutumia lugha ya Kiswahili.

Alifafanua kuwa Kiswahili ndiyo Lugha ya Taifa na inaeleweka na kutumika katika shughuli zote za maendeleo nchini.

"Pia, kutumika kwake kutasaidia katika upatikanaji wa haki nchini. Marekebisho haya yanakusudia kuimarisha mfumo wa upatikanaji haki kwa wananchi ambao ndiyo watumiaji wa sheria husika," alisema.

Aliongeza kuwa mapendekezo haya yamezingatia marekebisho yaliyofanywa kwenye Sheria ya Tafsiri za Sheria ambayo imeweka msingi wa lugha ya mahakama, mabaraza na vyombo vingine vyenye jukumu la kutoa haki kuwa ni Kiswahili.

"Pia, vyombo vya utoaji haki vinaweza kutumia Kiingereza pale itakapoonekana ni muhimu kufanya hivyo kwa maslahi ya utoaji haki kwa mashauri husika," alisema.

Dk. Mwigulu alisema endapo chombo cha utoaji haki kitalazimika kutumia Kiingereza, tafsiri ya mwenendo na uamuzi kuhusu shauri husika, itatolewa mara moja.

Alisema Waziri wa Sheria anapewa mamlaka ya kutunga kanuni ili kubainisha mazingira ambayo lugha nyingine zinaweza kutumika katika kutunga sheria au katika mfumo wa utoaji haki.

"Jaji Mkuu pia anapewa Mamlaka ya kutunga kanuni kwa ajili ya kutoa mwongozo ili kubainisha mazingira ya lugha ya Kiingereza inaweza kutumika katika utoaji wa haki," alisema.

Dk. Mwigulu alisema sehemu ya tatu na ya nne zinapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Mahakama za Migogoro ya Ardhi na Sheria ya Mahakama za Mahakimu ili kwa kufuta vifungu vinavyoweka sharti kuhusu lugha ya mahakama na sasa Kiswahili kitatumika.

**MAONI YA KAMATI**

Akisoma maoni ya Kamati ya Bunge ya Katiba na Sheria, Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Mohamed Mchengerwa, alisema kamati inashauri kuwekwa kwa kifungu kitakachompa waziri mamlaka ya kutangaza tarehe ya kuanza kutumika sheria hiyo.

Pia, alisema inashauri kuwapo kwa mwongozo maalum utakaobainisha namna mashauri yanayoendelea mahakamani hivi sasa yatakavyoshughulikiwa.

"Serikali ione ulazima wa kuhuisha sera ya lugha nchini kwa kuzingatia lugha ya kujifunzia kwenye taasisi za sheria, ili kuendana na mazingira ya sasa," alisema.

# Upofu waitesa familia

Na Maulid Mmbaga

FAMILIA yenye makazi yake Chanika jijini Dar es Salaam, inakabiliwa na tatizo la upofu, linalosababisha kushindwa kupata huduma za msingi ikiwamo chakula, mavazi na kusomesha watoto.

Katika mazungumzo na Nipashe akiwa nyumbani kwao jana, Mohamed Suleiman ambaye ni mtoto wa kwanza katika familia hiyo, alisema ana ulemavu huo na katika familia yao ya watoto 13, sita wana ulemavu wa macho.

Suleiman alibainisha kuwa hata binti yake wa kwanza, amejifungua mtoto mwenye ulemavu wa macho.

Alisema baba yao ambaye ndiye mwenye jukumu la kulea familia, ana ulemavu huo na kutokana na umri wake kuwa mkubwa, inamuwia vigumu kuihudumia ipasavyo.

Alisema baba yao anapata fedha kupitia shughuli za kidini na hazikidhi mahitaji ya familia hiyo.

Suleiman alisema wadogo zake wanasoma elimu ya dini tu kutokana na kushindwa kuwasomesha katika shule za kawaida kutokana na vikwazo walivyonavyo kuiuchumi.

"Kuwasomesha wadogo zangu shule za kawaida imeshindikana kwani niliwapeleka Shule ya Kilosa na Uhuru ya Kariakoo, lakini tukakutana na changamoto kwani kila kitu tuliambiwa tufanye wenyewe, kuwanunulia vifaa ikashindikana," alisema.

Aliongeza kuwa alishindwa kuwapeleka shule watoto hao kutokana na vifaa alivyotakiwa kuwanunulia kuwa ghali, akidai ni vinagharimu Sh. 300,000 ambazo hana.

Suleiman alisema historia ya ulemavu wa macho katika familia yao ilianzia kwa bibi yake ambaye ameshafariki dunia.

Alisema kuwa watu walimshauri kupeleka watoto kituo cha afya kwa ajili ya kufanyiwa uchunguzi wa kitabibu na mdogo wake wa mwisho alifanyiwa upasuaji, lakini hali yake ya kiafya ilizidi kudhoofika.

Suleiman aliiomba serikali na wananchi kuwasaidia chakula, mavazi, makazi na fedha kwa ajili ya kuwasomesha wadogo zake.



Wafanyabiashara mbalimbali wakiwa wamejikinga na mvua katika Soko la Kijiji cha Ijumbi, wilayani Muleba, mkoani Kagera, ikiwa siku ya mnada kijijini hapo, hivi karibuni. **PICHA: JUMANNE JUMAI.**

# Mradi wa maji Tanga kuwanufaisha mamia

Na Steven William, PANGANI

WAKAZI 400 wanaoishi katika Kijiji cha Ushongo, Kata ya Mwera wilayani Pangani mkoani Tanga, watafaidika na huduma ya maji safi na salama baada ya serikali kujenga mradi wa maji utakaonufaisha kijiji hicho kwa gharama ya Sh. mlioni 500.

Diwani wa Mwera, Gogo Yusuph, alitangaza neema hiyo mbele ya viongozi wa vyama na serikali walipotembelea na kukagua mradi huo katika kata hiyo.

Alisema serikali inajenga mradi wa maji kupeleka katika Kijiji cha Ushongo na utekelezaji wa mradi huo umefikia hatua nzuri ya kusambaza mabomba kupeleka kwa wananchi.

Yusuph alisema mradi huo unatarajiwa kugharimu Sh. milioni 500 mpaka kukamilika kwake, ukinufaisha wananchi takriban 400 wanaoishi katika kijiji hicho.

Katika hatua nyingine, Sh. milioni 86 zimetumika katika ujenzi wa mradi wa bweni Shule ya Sekondari Mwera.

Mkuu wa Shule hiyo, Jausia Mzirai, alisema serikali imeleta fedha Sh. milioni 86 kwa ajili ya mradi huo ambao tayari umekamilika na kinachosubiriwa sasa ni vitanda na kinahitajika kiasi cha Sh. milioni 14 kufanikisha hilo.

Alisema kuwa bado kuna ukosefu wa bwalo la chakula, lakini tayari ujenzi umeanza na wanahitaji fedha kwa ajili ya kukamilisha mradi huo.

Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Pangani, Rajabu Abdulrahaman, Katibu wa CCM Wilaya ya Pangani Mohamed Moyo, Katibu wa Wazazi Wilaya ya Pangani, Vicent Eunyo na Katibu Mwenezi wa CCM wilayani hapa, Salumu Kanyama, walitembelea miradi hiyo.

# SMS ya mwisho ya Nditiye kwa Spika

Na Augusta Njoji, DODOMA

SPIKA wa Bunge, Job Ndugai, ameongoza wabunge kuaga mwili wa Atashasta Nditiye, huku akisoma ujumbe wa simu wa mwisho aliotumiwa na Mbunge huyo wa Muhambwe (CCM).

Nditiye (pichani), alifariki dunia juzi katika Hospitali ya Benjamin Mkapa alikokuwa akipata matibabu baada ya kupata ajali katika eneo Nanenane jijini Dodoma, na mwili wake utasafirishwa leo mchana kwenda mkoani Kigoma kwa ajili ya mazishi.

Akitoa salamu za rambirambi, Spika Ndugai alisema alipochaguliwa kuwa mbunge katika uchaguzi wa mwaka jana, walikuwa hawajaonana na mwanzoni mwa mwezi huu, alimtumia ujumbe.

"Ninaomba 'ni-share' nanyi, "Mheshimiwa Spika, heri ya mwaka mpya 2021. Ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa sababu ya uhai na nimekuwa na ibada maalum mbili za kukuombea afya, hekima na amani kwa jinsi ulivyoniinua katika maisha yangu. Mungu aendelee kuwa upande wako siku zote. Amina!"

Spika Ndugai aliongeza: "Ninadhani ulikuwa unaniaga ndugu yangu na mimi nikamjibu, 'asante sana injinia, hakika tumekuwa pamoja, Mungu wetu ni mwema, hatatuacha kamwe', lakini leo tupo hapa tunamuaga mwenzetu, kweli maisha haya kila mmoja wetu ajiandae.

"Mwili utasafirishwa kesho (leo) mchana kuelekea Kibondo, Kigoma na tumetoa fursa ili wengine ambao wapo safarini washiriki mazishi," alisema.

Spika Ndugai alisema Nditiye alikuwa mpole na mwema na kwamba taarifa za ajali yake ziliwasikitisha wengi.

"Ni vigumu kusema hasa pale mmoja wetu anapopungua kwenye kundi, ni jambo linalosikitisha sana, lakini viongozi wa dini wametufundisha mtu aliyezaliwa na mwan-



amke, siku zake za kuishi si nyingi na maisha yake hujaa tabu. Tushukuru kwa kila jambo, tunashukuru kwa maisha ya Atashasta," alisema.

Alisema alipochaguliwa kuwa mbunge kwa mara ya kwanza, Nditiye alichaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii na kufanya kazi yake vizuri na kwa karibu na kushauriana naye kabla ya Rais kumteua kuwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alisema Nditiye alifanya kazi kubwa katika sekta ya mawasiliano ndani na nje ya Bunge.

"Lazima tukiri ameacha pengo maana ni mtumishi aliyejitambua na alikuwa akifanya kazi kwa uadilifu mkubwa," alisema.

Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. Bashiru Ally, alisema Nditiye alikuwa mchapakazi na miongoni mwa watu wa kwanza kufanya kazi alipoteuliwa kuwa Katibu Mkuu hasa katika uchaguzi mdogo wa Jimbo la Buyungu mkoani Kigoma.

HABARI KITAIFA

# Serikali kujenga sekondari 1,000

**Na Mwandishi Wetu, DODOMA**

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, amesema serikali itajenga shule mpya za sekondari 1,026 ili kukabiliana na upungufu uliopo.

Amesema kati yake, shule 26 zitakuwa za bweni zenye uwezo wa kupokea wanafunzi kati ya 1,000 hadi 1,500 kwa kila mkoa na zitajengwa kwa awamu tatu.

Majaliwa alitoa kauli hiyo jana alipowasilisha hotuba yake ya kuahirisha mkutano wa Bunge jijini Dodoma. Bunge limeahirishwa hadi Machi 30 mwaka huu.

Alisema shule nyingine mpya 1,000 za kutwa zenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 400 kwa kila shule, zitajengwa chini ya mradi wa maboresho ya elimu ya sekondari (SEQUIP) ambao utatekelezwa kwa muda wa miaka mitano (2020/21 - 2025/26).

Alisema Benki ya Dunia iliidhinisha mkopo wa kiasi cha Dola za Marekani milioni 500 (Sh. trilioni 1.2) kwa ajili ya mradi huo, na kwamba ukikamilika, utakuwa ni mwarobaini kwa tatizo la uhaba wa miundombinu ya shule za sekondari.

"Shule hizo zitajengwa kwenye kata 718 zisizo na sekondari za kata na kwenye maeneo yaliyoelemewa na idadi kubwa ya wanafunzi.

"Hivyo basi, nitumie nafasi hii kuwaelekeza viongozi na watendaji wa serikali za mitaa, wasimamie kikamilifu utekelezaji wa mradi huu ili kufikia malengo yaliyokusudiwa," alisema.

Waziri Mkuu alisema katika kipindi cha Julai 2020 hadi Januari 2021, vijana 10,178 wamepatiwa mafunzo na kutathminiwa ujuzi walioupata nje ya mfumo rasmi wa mafunzo nchi nzima ambapo vijana 9,736 wamefaulu na kupatiwa vyeti na Mamlaka ya Mafunzo na Ufundi Stadi (VETA).

Alisema vyeti hivyo vinawawezesha vijana hao kutambulika, kujiendeleza kiujuzi, kujiajiri na kupata kazi katika taasisi na kampuni mbalimbali. "Vijana hao ni wenye ujuzi katika fani za uashi, useremala, ushonaji, ufundi bomba, uchomeleaji na uungaji vyuma, ufundi magari, ufundi umeme, ukarabati wa bodi za magari, upishi na uhudumu katika hoteli.

Alisema serikali pia imekamilisha ujenzi wa maghala 14 ya kuhifadhia mavuno katika skimu za umwagiliaji za Ngana na Makwale (Kyela), Magozi na Tungamalenga (Iringa), Mbuyuni-Kimani, Ipatagwa, Kongolo-Mswiswi na Motombaya (Mbarali), Lekitatu (Arusha), Mombo (Tanga), Uturo (Mbeya), Bagamoyo (Pwani), Mkindo na Mkula (Morogoro).

"Katika hatua ya kuongeza mnyororo wa thamani kwenye uzalishaji wa mazao ya kilimo, kati ya maghala hayo, maghala sita yamewekewa na vinu vya kukobolea mpunga," aliongeza.



Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Viwango nchini (TBS), Dk. Athumani Mgenya (kulia), akikabidhi cheti cha Ubora wa Bidhaa kwa Meneja Mkuu wa Kiwanda cha kutengeneza magari cha GFA cha Kibaha, mkoani Pwani, Ezra Mereng, wakati wa sherehe ya kutoa vyeti kwa kampuni na wajasiriamali waliokidhi vigezo katika uzalishaji, jijini Dar es Salaam jana.. **PICHA: MIRAJI MSALA.**

## Sekta binafsi yaitwa kuwekeza katika kilimo

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

SERIKALI imesema inafanya jitihada za kuhakikisha sekta binafsi inashiriki kikamilifu kwenye ukuzaji wa kilimo nchini, hususani katika masoko ya mazao ya nafaka, ili kusaidia wakulima kujikwamua kiuchumi.

Waziri wa Kilimo, Prof. Aldof Mkenda, aliyasema hayo wakati akifungua mkutano wa wafanyabiashara wa mazao ya nafaka uliofanyika jijini hapa.

Prof. Mkenda alisema serikali inawasikiliza wafanyabiashara wanahitaji nini kifanyike ili kupiga hatua katika mazao ya nafaka nchini.

"Unakuta tuna mchele mzuri tu na mazao mengine ya biashara ya nafaka, lakini ninajiuliza mbona watu hawaendelei ilhali bidhaa wanayolima ni nzuri? Prof. Mkenda alihoji.

Alisema wafanyabiashara waliohudhuria mkutano huo, wanapaswa kutumia nafasi hiyo kujadili mambo ya msingi kuijenga sekta hiyo na kuwainua wakulima na wafanyabiashara wa mazao ya nafaka.

"Washiriki wa mkutano huu tumieni fursa hii kujadili mambo muhimu ambayo mtaiambia serikali ifanyeje ili sekta ya kilimo ipande juu kiuchumi," alisema.

Alilishukuru Shirika la Kilimo Afrika (AGRA) kwa kuandaa mkutano huo ambao utasaidia kuibua mambo muhimu ya msingi ambayo yatasaidia sekta hiyo na kuinuka zaidi uchumi.

Alisema tatizo kubwa liko katika uzalishaji kutokana na watu kushindwa kukua kiuchumi, hivyo akawataka wafanyabiashara kutumia mkutano huo kujadili mambo muhimu ambayo yatafanyiwa kazi.

Alisema wizara husika inahitaji kuona wakulima wanafanya vizuri katika kilimo na ndiyo maana wamekubali kushiri katika mkutano ambao utaleta mafanikio makubwa katika sekta hiyo.

# TBS yawaita wafanyabiashara kusajili bidhaa

**Na Mwandishi Wetu, Arusha**

SHIRIKA la Viwango (TBS) limewataka wafanyabiashara kujitokeza kusajili bidhaa na majengo ya vyakula na vipodozi ili kuwawezesha kufanya shughuli zao kwa kukidhi matakwa ya sheria za nchi na kulinda afya za walaji.

Wito huo ulitolewa jana na Ofisa Uhusiano wa TBS, Neema Mtemvu, kwenye Maonyesho ya Nne ya Mifuko na Programu za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi yaliyoanza Februari 7 mwaka huu hadi 13 jijini Arusha yakiandaliwa na Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC).

Shirika hilo linashiriki maonyesho hayo ili kutoa elimu ya viwango kwa wananchi, wajasiriamali, wafanyabiashara na wadau mbalimbali na msisitizo wao mkubwa ni ujenzi wa Tanzania ya viwanda na kukua kiuchumi.

"Tunatoa wito kwa wanaofika kwenye maonyesho haya kusajili bidhaa na majengo ya vyakula na vipodozi kwa mujibu wa sheria ambayo imetokana na mabadiliko ya Sheria ya Fedha ya Mwaka 2019," alisema Mtemvu.

Sheria hiyo ilirudisha majukumu ya usimamizi wa usalama na ubora wa vyakula na vipodozi kwa TBS kutoka kwa iliyokuwa Mamlaka ya Dawa na Chakula (TFDA).

"Kwa hiyo, usajili wa bidhaa, majengo ya vyakula na vipodozi ni matakwa ya kisheria ili kuwawezesha kufanyabiashara zao urahisi," alisema Mtemvu wakati akitoa ufafanuzi wa masuala mbalimbali kwa wananchi waliotembelea banda la shirika hilo kwenye maonyesho hayo.

Alisema usajili majengo ya biashara unawapa wafanyabiashara uhakika wa kutunza bidhaa na kwamba wanasajili jengo kulingana na bidhaa zinazoenda kuhifadhiwa humo.

Mtemvu alisema eneo linalohusika ni bidhaa za chakula na vipodozi, akifafanua kuwa usajili wa vipodozi unalenga kuhakikisha vipodozi vilivyopigwa marufuku kwenye soko la Tanzania, haviingizwi nchini kutokana na kuwa na viambata sumu.

Alitoa wito kwa wajasiriamali kujitokeza kwa wingi kuthibitisha ubora wa bidhaa zao TBS bure, kwa kuwa gharama hizo zinalipwa na serikali kwa lengo la kuwawezesha kufanyabiashara.

Alisema wanachotakiwa kuwa nacho ni barua ya utambulisho kutoka SIDO na baada ya hapo wakifika TBS, mchakato unaanza mara moja. Alisema wamefurahishwa na mwitikio mkubwa wa wananchi kwenye maonyesho hayo.

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Rais ameonyesha ukubwa wa rushwa, TAKUKURU iamke

**RAIS** John Magufuli, wiki hii alifanya ziara ya kikazi katika Mkoa wa Morogoro pamoja na mambo mengine, alizindua soko kuu la manispaa ya Morogoro alilililoliita Soko la Chifu Kingalu na kuzindua viwanda vilivyojengwa.

Katika ziara hiyo, Rais alizungumza mengi ikiwamo kukemea vitendo vya rushwa ambavyo alisema vimekithiri kwa baadhi ya watendaji wa Manispaa ya Morogoro na ndani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) hasa wakati wa mchakato wa uchaguzi wa Meya. Kutokana na kuwapo kwa tuhuma hizo, aliweka bayana kwamba katibu wa CCM Mkoa wa Morogoro, amesimamishwa kazi.

Licha ya hatua hizo kuchukuliwa, Rais alisikiliza malalamiko kutoka kwa baadhi ya wafanyabiashara wa soko hilo jipya na baadhi kumweleza kuwa mmoja wa watumishi wa manispaa, alikuwa akiwatoza Sh. 50,000 kama kodi ya pango la kizimba wakati tozo halisi kwa mwezi ni Sh. 20,000. Kutokana na tuhuma hizo, Rais aliagiza mfanyakazi huyo azirejeshe fedha hizi kwa wafanyabiashara hao na kuchukuliwa hatua zinazostahili.

Rais magufuli hakuishia hapo kwani alionyesha kukasirishwa na kasi ya baadhi ya watendaji wa Wizara ya Viwanda na Biashara pamoja na Ofisi ya Rais (Uwekezaji) kutokana na ucheleweshaji wa vibali na urasimu usiio wa lazima.

Kutokana na hali hiyo, Rais aliwataka watendaji hao pamoja na mawaziri waliopewa dhamana ya kuongoza wizara hizo, kubadilika na kwenda na kasi zaidi ili kuhakikisha azma ya uanzishwaji wa viwanda pamoja na uwekezaji inafanikiwa. Kadhalika alisema hatakuwa na mswalie mtume na watendaji hao na kwamba kama hawatabadilika atawafukuza na wasimlaumu kwa uamuzi huo.

Bila kuuma meneno, Rais Magufuli alisema baadhi ya watendaji katika wizara hizo wamekuwa wakifanya ucheleweshwaji na kuwazungusha wawekezaji bils sababu.

Alichokizungumza Rais mkoani Morogoro ni kitu cha wazi kwa sababu pamoja na hatua mbalimbali kuchukuliwa baadhi ya watendaji wa serikali katika wizara na taasisi nyeti, wamekuwa wakiendekeza vitendo vya rushwa, hivyo kukwamisha huduma kwa wananchi na maendeleo ya taifa kwa ujumla.

Katika maeneo ambako miradi inatekelezwa, kumekuwa na malalamiko kuhusu rushwa kutoka kwa baadhi ya watendaji. Hata kwenye ugawaji wa maduka ya biashara katika sehemu zenye huduma kumekuwa na vitendo hivyo.


Mfano halisi ni katika stendi mpya ya mabasi ya mikoani iliyojengwa eneo la Mbezi Luis, jijini Dar es Salaam. Katika eneo hilo, kulitangazwa zabuni kwa ajili ya ukodishaji wa vizimba vya biashara na kukawapo madai kwamba zabuni hiyo ilitangazwa kama utaratibu lakini waliopangishwa walishapewa kabla hata havijamalizika ujenzi.

Rais Magufuli ameweka bayana kwamba licha ya serikali yake kupambana ma rushwa kwa nguvu zote, bado kuna baadhi ya watumishi wanaendelea kuomba na kupokea rushwa katika maeneo mbalimbali.

Kwa kauli hiyo ya Rais, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) inapaswa kuzinduka na kubadili mbinu ya kukabiliana na vitendo hivyo viovu kwenye taasisi mbalimbali za huduma na biashara.

Tunasema hivyo kwa sababu watu wanaojihusisha na rushwa ni sawa na kirusi cha ugonjwa fulani, hivyo kila mbinu inapobadilika ya kupambana nacho, pia hutafuta namna ya kujibadili ili kutodhurika na dawa husika. Kwa mantiki hiyo, mbinu zaidi na nguvu zaidi zinapaswa kutumika katika kukabiliana na ufisadi na rushwa katika taasisi za serikali na binafsi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Sabato Kasika

## Muungwana Lazima Nilonge

## Jamii ibadilike na kushiriki kutokomeza mimba utotoni

**KILA** kukicha, kumekuwapo na taarifa za wanafunzi kukatisha masomo kwa sababu ya mimba au ndoa za utotoni, ambavyo vyote huchangia kuwafanya wakatishe ndoto zao za kimaisha hususani elimu.

Ziko sababu ambazo hutajwa kuwa chanzo cha mimba na ndoa hizo ikiwamo tamaa za wazazi na walezi kutaka mali, ukosefu wa elimu ya afya ya uzazi na umbali wa shule na hasa sekondari za kata.

Umbali unasababisha wanafunzi kutembea muda mrefu kufuata elimu na kujikuta wakikumbana na vishawishi njiani, ambavyo wakati mwingine vinasababisha waingie kwenye mahusiano na hivyo kupata mimba.

Hizo ndizo sababu zinazoendelea kutajwa huku kukiwa na juhudi mbalimbali zinazofanywa na serikali kwa ajili ya kukabiliana na tatizo hilo ambalo ni kikwazo kwa maendeleo ya elimu ya mtoto wa kike.

Kwa ujumla ni kwamba mimba bado zimeendelea kuwapo na sababu ni zile zile ambazo hazijapatiwa ufumbuzi wa kudumu, hali ambayo sasa ni muhimu wadau wote kushirikiana katika vita hiyo.

Mabweni katika sekondari za kata yanaweza kuzuia mimba kwa wanafunzi, lakini tatizo ni kwamba siyo shule zote zina mabweni, hivyo kuna haja ya kuongeza kasi katika ujenzi wa mabweni.

Kuwapo kwa mabweni kwa ajili ya wanafunzi wa kike kunaweza kuwapunguzia vishawishi, ambavyo wanakutana navyo njiani ikiwamo lifti za bodaboda wanapotembea umbali mrefu kwenda shule au kurudi nyumbani.

Inawezekana mwanafunzi akakataa lifti, lakini akibembelezwa, mwishowe akadhani dereva wa bodaboda ana nia njema ya kumsaidia na kumbe ndiyo anajiingiza katika mdomo wa mamba.

Hivyo, umefika wakati sasa jamii kushiriki kikamilifu katika kufanikisha ujenzi wa mabweni ili kumaliza tatizo hilo ambalo linasababisha pia wanafunzi kupanga kwenye 'magheto', ambayo nayo bado ni tatizo kwao.

Kwenye suala la elimu ya afya ya uzazi, bado kila mzazi ana jukumu la kumfundisha mtoto wake kujitambua kadri anavyokua ili hatimaye aweze kukabliana na changamoto zilizo mbele yake.

Lakini bahati mbaya wazazi wa siku hizo, wako 'bize' kuhangaikia maisha na kuwaacha watoto wakijilea wenyewe, na matokeo yake wanajikuta kwenye vishawishi na kushindwa kukabiliana navyo.

Wanaposhindwa kukabiliana na vishawishi, mwisho wa siku ni kujiingiza kwenye mambo ya uhusiano na kujikuta wakipata mimba, ambazo hazikutarajiwa na kulazimika kukatisha masomo.

Vilevile kuna suala la umaskini wa kipato kwenye baadhi ya familia, nalo linasababisha baadhi ya wazazi kuwa na tamaa ya kupata mali kwa wanawageuza watoto wa kike kama mitaji wao.

Hili nalo wakati mwingine linaambatana na mila na utamaduni wa baadhi ya makabila hapa nchini, ambavyo ni jambo la kawaida mtoto wa kike kupata mimba kukubali kupewa chochote ili mambo yaishe kimyakimya.

Mtu akichukua muda wa kutafakari sababu hizo zinazoendelea kuchangia kuwapo kwa tatizo la mimba kwa watoto wa kike, atabaini kuwa ziko ndani ya uwezo wa jamii, ila haijaamua kubadilika na kuchukua hatua.

Ni kweli kwamba wapo wapo baadhi ya watoto wa kike walioshindikana, lakini ukubwa wa tatizo la mimba usingekuwa wa kiasi hicho ambacho kimekuwa kikitajwa kama hatua zingechukuliwa inavyotakiwa.

Hebu fikiria, kuna wilaya moja ambayo kwa mwaka jana, jumla ya wanafunzi 2, 177 walipata mimba, sasa kama kila wilaya nchini itakuwa na idadi hiyo ya mimba ni wanafunzi wangapi watakatisha masomo?

Kuna haja kwa jamii kutafakari na kisha kuchukua hatua za kushiriki kikamilifu katika kutafutia ufumbuzi matatizo ambayo yamekuwa yakitajwa kuchangia ongezeko la mimba kwa wanafunzi na ndo za utotoni.

Ikumbukwe kuwa shule za msingi na sekondari za serikali ni umma, hivyo umma wenyewe una wajibu wa kuzihudumia ikiwamo kushiriki katika ujenzi wa mabweni pamoja na miundombinu mingine.

Jamii ikitambua hilo, itakuwa ni rahisi pia kuwakazania watoto kusoma na kuepuka kuwaozesha au kukubali kupokea fedha kutoka kwa wale wanaowapa mimba na kuwavurugia ndoto za baadaye.

SAFU

FIKRA MBADALA

# Hatuna haja wala sababu kukionea aibu Kiswahili



Nkwazi Mhango, Canada

MWALIMU Julius Nyerere alipoamua Kiswahili kuwa lugha ya taifa la Tanzania huru, wengi hasa majirani zetu, tena wengine waliopigania uhuru naye, walimcheka. Hata hivyo, Nyerere alishikilia uzi ule ule ingawa naye hakukitangaza Kiswahili vizuri.

Hakukitumia ziarani nje au kuhutubia vikao vya kimataifa kama wafanyavyo viongozi wa mataifa yanayotumia lugha zao asilia kama lugha za taifa. Leo tuna mataifa yanayojivunia kujua Kiingereza bila kukijua huku yakisema Kiswahili ni lugha zao za taifa. Lugha ni nyenzo ya mtu kuiona na kuielezea dunia yake.

Utafiti unaonyesha kuwa watu wanaelewa zaidi kwenye lugha mama kuliko lugha za kigeni. Najua Kiswahili si lugha mama ya Watanzania wote. Angalau ni lugha ya pili yenye kukaribiana na lugha mama ikilinganishwa na lugha za watawala wetu wa kikoloni ambao hatuna ukaribu kimila au kwa lolote.

Uhuru maana yake ni ile haki ya binadamu kujiamulia bila woga kufanya kile unachoona kinafaa kisheria kama mtu binafsi, jamii au nchi. Kwa kuzingatia dhana hii, Rais John Magufuli alipoingia madarakani aliamua kukanyaga nyayo za Mwalimu bila aibu wala woga tena kindakindaki kwa kuamua kutumia Kiswahili kama lugha yake ya mawasiliano katika kila shughuli ya kitaifa anayofanya kama Rais.

Hata hivyo, uamuzi huu, kutokana na mabaki na mtindio wa kikoloni, haukupokewa na Watanzania wote. Wako waliombeza kwa maneno mengine wakidai hajui Kiingereza. Magufuli aliwashangaa hawa kwa kuhoji aliwezaje kupata shahada mbili za juu moja ya uzamili na nyingine ya uzamivu bila kujua Kiingereza wakati masomo yote yalifanyika kwenye lugha hiyo?

Hivi karibuni, akihutubia sherehe za kuadhimisha miaka 100 ya Mahakama, alisema wazi alivyojiamini na kuisimamia lugha ya Kiswahili pamoja na kukejeliwa kuwa hajui Kiingereza. Kuonyesha alivyodhamiria, Magufuli alimpandisha cheo Jaji wa Mahakama Kuu kanda ya Musoma, Zephrine Galeba, kuwa Jaji wa Mahakama ya Rufani kwa uzalendo wake wa kutoa hukumu kwa Kiswahili jambo ambalo, licha ya kumvutia Rais, lilimpa imani kuwa Idara ya Mahakama itabadilika na kuanza kuenzi na kutumia Kiswahili katika kazi zake. Je, hili litawezekana bila kutungiwa sheria? Nchi za kiafrika kuogopa kutumia lugha zao ni aina fulani ya ukoloni ambayo inapaswa kuangaliwa upya. Nadhani haya ndiyo matokeo ya dini za kigeni zilizowafundisha waswahili kuwa karibu kila kitu chao ni cha shetani isipokuwa vyakula vyao na wanyama wao. Ndiyo maana watu wenye mawazo ya kikoloni tena ya kujitakia wanaogopa lugha na majina yao.

Ndiyo, tunahitaji Kiingereza kama lugha inayotumika sana duniani. Hili lisitupe unyonge wa kuogopa lugha zetu asilia au za taifa zenye asili ya Afrika kama Kiswahili. Nikiwa Kenya kipindi fulani, majirani zangu walisema mimi si Mtanzania kwa vile naongea Kiingereza kizuri.

Niliwajibu mbona Nyerere alikiongea vizuri kuliko rais wao wa awamu ya pili hata wa awamu ya kwanza? Niliwasuta kuwa nawasikitikia kwa vile hwakuwa wakijua ima kiingereza au Kiswahili wakati mie navimudu vyote bila wasi wasi.

Kama tutakuwa wakweli, watu wetu wengi kiingereza kinawapa taabu si kwa sababu hawakijui bali hawakuandaliwa kukijua tokana na fikra huru za baba wa taifa. Juzi nilimsikia mkuu fulani wa wilaya akisema visibility studies badala ya feasibility studies. Hii inaweza kuonyesha ni kwa nini tunahitaji lugha yetu ambayo watu wataitumia kwa kujiamini. Hata wanaojifisia kujua kimombo wana matatizo kibao.

Mfano, ukimwambia Mkikuyu pale Kenya aseme neno pond atakwambia pod. Ukimwambia Mmeru aseme neno pond atasema mpond. Uganda nako utasikia exichuse me badala ya excuse me. Pale Nigeria wanasema broda badala ya brother. Afrika Kusini wanasema struggal wakimaanisha struggle. Hii ni kuonyesha namna waswahili tunavyoweza kutumia lugha zetu na mambo yakaenda.

Ni ushahidi tosha kuwa, pamoja na kutumia lugha za wenzetu, bado tunazibukanya au kuboronga huku tukijisifu tunazimanya. Huku Ulaya ukiongea mfano Kiingereza, hutaacha kusikia kuwa una accent au lafudhi kukuonyesha kuwa hii si lugha yako na huwezi kuimilki kama wao. Huwa najiuliza. Kama nina lafudhi na unajua, una haja gani ya kuniambia kama si ubaguzi tu wa kawaida na kujiamini kwa wale wanaojiona ndiyo wenye lugha?

Kama tutajivunia lugha za watawala wetu wa kikoloni basi tujivunie na zetu. Hii inanikumbusha Wasudan ya Kaskazini ambao huonea fahari kiarabu hadi kujiita Waarabu wakati Waarabu wakiwaita watumwa yaani abid kutokana na kujikana na mila na lugha zao.

Naamini kuwa unapojikana na wengine watakukana. Usiopojiamini hutaaminiwa na usipojipenda hutapendwa. Kimsingi, utachuliwa na wengine kama unavyojichukulia. Na hii ndiyo siri ya nchi za magharibi kujiamini hata pale zinapokuwa zinatufunza vitu visivyoendana na utamaduni na imani zetu waka kuingia akilini.

Ndiyo maana Wasudan hata wanaposhiriki kwenye mikutano ya nchi za kiarabu au kwenda kufanya kazi kwenye nchi hizo wanaonyeshwa wazi kuwa wao ni waswahili na si waarabu. Ukitaka kujua mbuzi au kondoo ni kondoo au mbuzi, mpeleke kwa wale wanaosema ni mbuzi au kondoo wenzake. Wakimpokea basi ni mwenzao.

Hata wanyama pamoja na ufinyu wao wa akili bado hawawezi kumkubali mnyama ambaye si mwenzao. Mbuzi watamkubali mbuzi na kumkataa kondoo na kondoo kadhalika watamkubali kondoo na kumkataa mbuzi kama ambavyo waarabu hufanya kwa wasudani.

Nimalizie kwa angalizo na ushauri. Kuenzi lugha zetu hakuna maana ya kuzikimbia lugha za watawala wetu hasa kutokana na ukubalikaji wake duniani. Tunaweza tukaendelea kuzitumia bila kukimbia lugha zetu. Mbona mataifa kama Japan Korea Kusini na Uchina yaliyoendelea yanatumia lugha zao asili na yameendelea?

Hatuna haja ya kuogopa kutumia Kiswahili katika mambo yetu ya kitaifa; ni lugha sawa na nyingine yenye uwezo kuwa na dhana zote tunazodhani zinapatikana kwenye lugha za kigeni tu.

MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Magufuli piga kazi waachie Kiingereza chao



Na Joseph Kulangwa

“NIMEFANYA PhD (shahada ya uzamivu) bado wanasema sijui Kiingereza, na nikaka mwaka mzima Uingereza, sijui nilikuwa nazungumza Kisukuma kule! Wakasema sijui Kiingereza, niliamua kuzungumza Kiswahili na kuki-promote (kukitangaza), kwa sababu ni lugha iliyoachwa na Baba wa Taifa.”

Hiyo ni kauli ya Rais John Magufuli alipokuwa akizungumza kwenye maadhimisho ya Miaka 100 ya Mahakama Tanzania, alipokuwa akishajihisha umuhimu wa Kiswahili kutumiwa mahakamani, hususan katika uandishi wa mwenendo wa kesi na hukumu.

Si mara ya kwanza Rais analalamika dhidi ya wanaomzushia kuwa haujui Kingereza, eti kwa sababu tu hakitumii kwenye shughuli zake mbalimbali ikiwa ni pamoja na hotuba. Mimi ningemwomba Rais awapuuze wanaomlaumu kwa hilo.

Kabla sijasema nalotaka kulisema hapa, natangaza maslahi binafsi kwake kwamba mbali na kuwa ni Rais wangu na mwanachama mwenzangu, nimesoma naye darasa moja Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), hivyo namfahamu.

Miongoni mwa waliokuwa marafiki zake name najigamba kuwa mmoja wao na hataalipokuwa ameingia kwenye siasa na mpaka kuwa Waziri na sasa ni Rais, ameendelea kuwa rafiki yangu, kwa sababu madaraka si ukuta wa kutuzuia. Hivyo namfahamu fika.

Namfahamu alivyo nguli katika kuzungumza lugha mbalimbali, zikiwamo za makabila ya ndani ya nchi, nikiwa na uhakika kabisa wa Kisukuma, Kihaya, Kisubi na hata Kikerewe na ndiyo sababu baadhi ya marafiki zake walikuwa wa makabila hayo.

Tukiwa pamoja UDSM, tulishiriki naye semina za kimasomo darasani, ambazo ziliendeshwa kwa Kiingereza na hata kufanikiwa kumaliza masomo yetu ya Shahada ya Kwanza mwaka 1988 bila‘ kuvutwa shati’ wala ‘kudisco’. Mitihani yote ikifanywa kwa Kiingereza.

Akasoma Shahada ya Uzamili kwa Kiingereza, ya Uzamivu kwa Kiingereza, akafundisha sekondari kwa Kiingereza, amekuwa mbunge, naibu waziri na waziri, kote huko akiwasiliana kwa Kiingereza kimaandishi na kimazungumzo. Vivyo hivyo kwenye urais.

Sasa kaugua ugonjwa gani Yarabi, hivyo sasa asiweze kuwasiliana kwa Kiingereza? Au yeye kutaka kuimarisha na kukienzi Kiswahili ni dhambi? Rais anayeongoza Watanzania ambao asilimia kubwa ni Waswahili atakiwe kuzungumza Kiingereza? Kinatusaidia nini Watanzania?

Kama ilikuwa lazima tuwe na Rais wa aina hiyo, basi ni vyema tukachaguliwa Rais na Waingereza na atoke London. Nadhani Watanzania tufike mahali hata kama tu wapinzani, kukumbatia masuala yenye uzito na umuhimu kwa jamii, kuliko haya madogo yasiyo na tija.

Tunaona serikali yake inayoyafanya, kwa sababu reli ya kisasa haijengwi kwa Kiingereza, Bwawa la Umeme la JK Nyerere halijengwi kwa Kiingereza, si hospitali, zahanati wala vituo vya afya.

Hivi siku Rais Magufuli akiamua kuitisha mkutano wa hadharaa kazungumza Kiingereza mwanzo mwisho, atasemwaje? Hawatasema amedharau Kiswahili wakati anazungumza na Watanzania?

Wanaotaka Rais wa Kiingereza wasubiri muhula huu wa mwisho wa miaka mitano uishe ili tuone kama kweli Watanzania watataka Mwingereza awaongoze ili awe anawasiliana nao kwa Kiingereza.

Tumwache Rais ajenge nchi, tumpe ushirikiano atuokoe na magumu tunayopitia ili ifike siku Waingereza nao watuone tunastahili kujivunia Kiswahili, ambacho ndicho kinachotuletea maendeleo tunayoyashuhudia hivi sasa. Dk. Magufuli piga kazi tuko nyuma yako.

Kuna usemi wa Kifaransa, kwamba ‘Le chien a bois la caravan e passe (kubwe ka kwa mbwa hakuzuii lori kupita). Waingereza- Wabongo endeleeni na Kiingereza chenu. Alamsiki!

SAFU

## KONA YA UKWELI

# Rais Magufuli amewaumbua wapambe maslahi, wapinzani



Na Thobias Mwanakatwe

MKUTANO wa Pili wa BUNGE la 12 ambao lilianza vikao vyake Februari 2, mwaka huu, na kuhitimishwa jana, limezua mjadala mkubwa hususani kwenye mitandao ya kijamii baada ya wabunge wawili kutoa hoja kwamba Rais John Magufuli aongezewe muda wa kukaa madarakani.

Mbunge wa Makambako (CCM), Deo Sanga, maarufu kama Jah People, Februari 3, mwaka huu, alirudia kauli yake ya kutaka Rais Magufuli aongezewe muda wa kukaa madarakani na kuungwa mkono na Mbunge wa Kyela (CCM), Ally Jumbe, maarufu Kinanasi ambaye alilitaka Bunge litoe tamko juu ya suala hilo.

Hii ni mara ya pili kwa Sanga kutoa hoja kama hiyo. Alifanya hivyo katika Bunge la 11 zaidi ya mara mbili akitaka Rais Magufuli anayemaliza muda wake wa miaka 10 mwaka 2025 kuongezewa muda ili aendelee kukaa madarakani huku akitaja sababu mbalimbali.

Mbali na Sanga, Mbunge wa zamani wa Chemba (CCM), Juma Nkamia, na aliyekuwa Mbunge wa Nkasi Kaskazini, Ally Keissy, nao waliwahi kuzungumzia suala la Rais Magufuli kuongezewa muda.

Pamoja na wabunge hao na watu mbalimbali kutoa maoni yao, Rais Magufuli amekuwa akikaririwa mara kadhaa akisema hawezi kuongeza muda. Lakini kinachoonekana ni kwamba baadhi ya wabunge wa CCM kama wameziba pamba masikioni. Hawataki kumwelewa mheshimiwa Rais msimamo wake huo.

Suala hili linaenezwa kwa hamasa na upinzani na taasisi za nje za propaganda, kwamba Rais Magufuli alikuwa na ajenda ya siri ya kujiongezea muda baada ya kipindi chake cha pili cha urais kwisha.

Pamoja na Rais Dk. Magufuli kusema mara kadhaa kuwa urais wa nchi ni kazi ngumu ya kujituma, hivyo hataongeza hata dakika moja kukaa Ikulu, bado tetesi ziliendelea kutokana na baadhi ya viongozi wa CCM, hasa baadhi ya wabunge, kuliingiza suala hilo bungeni na kuzua mitaani tetesi za kutumwa kufanya hivyo.

Nampongeza Rais kwa kuonyesha kukerwa na kampeni hiyo iliyoibuka tu kama uyoga bungeni bila kuvihusisha vyombo vya chama vya uamuzi.

Kwa hatua yake ya kuzima kampeni hiyo ya wapambe maslahi, hoja pekee waliyobaki nayo wapinzani na taasisi za nje ni kuikosoa serikali kwa madai ya uvunjaji wa katiba.

Rais anapigwa vita na wahafidhina wa ndani na nje kutokana na kazi kubwa aliyoifanya kipindi chake cha kwanza cha miaka mitano.

Si siri kuwa idadi kubwa ya Watanzania inamuunga mkono Rais Magufuli na kumwombea afanye makubwa zaidi. Pia si siri kuwa kutokana na uongozi wake, dunia inatuangalia kwa jicho tofauti.

Si siri vilevile kuwa Dk. Magufuli akiendelea na kasi ile ile ya kipindi chake cha kwanza, ataacha alama isiyofutika ya uongozi uliotukuka si tu Tanzania wala Afrika, bali dunani kote.

Hili wakubwa wanalijua na linawasumbua, hivyo mkakati ni kumvuta shati kwa kutumia vyombo vyao vya propaganda, wapinzani uchwara na wapambe maslahi. Lengo ni kuzuia Magufuli wengine wasizaliwe Afrika na kile Prof. Lumumba anachokiita "The Magufification of Africa".

Hatua hizi za kizalendo na kiuongozi za Rais Magufuli, kwa kiasi kikubwa zimewanyima watu fursa ya 'biashara uchwara.

MUNGU IBARIKI TANZANIA,
MUNGU MBARIKI RAIS WETU

***Kwa maoni na ushauri tumia barua pepe mwanakatwe2015@gmail.com***

## DARASA LA NDOA

# Kanuni 10 za kukabili migogoro ya ndoa



Na Mch. Dk. Enock Mlyuka

WANANDOA wengi hawana ufahamu wa namna ya kukabili migogoro ya ndoa pale inapojitokeza katika ndoa zao. Katika toleo lililopita, tulijifunza suala zima la migogoro ya ndoa, faida na athari zake.

Kama nilivyoeleza katika makala iliyopita kuwa, faida za migogoro ya ndoa ni chache zaidi kuliko athari zake. Kwa kuzingatia ukweli kwamba athari za migogoro ya ndoa ni kubwa, kuna umuhimu kwa wanandoa kujifunza namna bora ya kukabili na kutawala migogoro yao ya ndoa.

Zifuatazo ni kanuni 10 za namna ya kukabili migogoro ya ndoa;-

**BADILIKA ILI KUBADILI**

Watu wengi ni wepesi wa kuona makosa ya wengine kuliko yao kwa sababu ya kutokujitambua. Hali hii imesababisha watu wengi kukosa utayari wa kubadilika na matokeo yake ni kubomoa uhusiano. Kabla hujamhukumu mwenzako, jiulize wewe una nafasi gani katika tatizo au mgogoro huo.

Je, wewe ni sehemu ya suluhisho au chanzo cha tatizo? Lazima uwe mkweli katika kutafuta ufumbuzi wa tatizo. Ni muhimu ubadilike kwanza kabla ya kutaka kumbadili mwingine kwani katika ndoa hakuna tatizo lisilochangiwa na wanandoa wote wawili ama kwa kauli au matendo.

Kwa hiyo, ili kutatua na kutawala mgogoro wenu, badili mtazamo ulio nao juu ya mwenzako au suala, ndipo mtazamo utakubadili. Ni vigumu sana wanandoa kuleta mabadiliko chanya katika uhusiano wao kama hawako tayari kubadilika.

**DHAMIRA YA KUTAKA SULUHU**

Pamoja na changamoto zilizopo, uhusiano wa ndoa si wa kulazimika kuwapo, bali kudhamiria kuwapo. Imejitokeza tabia kwa baadhi ya wanandoa kutokupenda suluhu. Mara nyingine, unakuta wanandoa wanakuja kutaka ushauri huku wakiwa wameishafanya uamuzi wa kuachana na si kutengeneza uhusiano wao.

Roho ya kutaka suluhu inakuwa imekufa. Suluhu katika mgogoro hupatikana pale wanandoa wanapokuwa na dhamira ya dhati ya kutaka suluhu. Wanandoa wakiamua na kuwa na nia na lengo moja la kutaka upatanisho, wanayo nafasi kubwa ya kumaliza mgogoro. Kwa mantiki hiyo, wanandoa wanapaswa kujenga tabia na utamaduni wa kupenda mazungumzo ili kuondoa tofauti zao.

Wanandoa wengi hawazungumzi, bali wanaongea. Ukiona udhaifu kwa mwenzako, usimweleze mtu wa tatu. Tafuta namna ya kuzungumza na mwenzako kwanza kwani upo ili umsaidie.

**KUCHAGUA MUDA UNAOFAA**

Si muda wote unafaa kwa mazungumzo. Chagua muda mzuri unaofaa. Mambo mazito hayazungumzwi usiku wa manane kwani huo ni wakati wa mwili na akili kupumzika kwa sababu ya uchovu wa shughuli za kutwa nzima. Yafaa mazungumzo yafanyike wakati watu wakiwa hawajachoka akili na mwili. Muda mzuri mara nyingi ni ule wa alfajiri au ule ambao utaleta ufanisi wa mazungumzo.

Katika kuangalia muda muafaka wa kufanya mazungumzo, ni muhimu pia kuangalia hali ya mwenzako (mood). Kama ana hasira, subiri hasira zake zishuke ndipo mazungumzo yafanyike kwani hasira huchochea ugomvi. Tengeneza mazingira ya kutuliza hasira za mwenzako. Wakati mtu ana hasira si mwafaka kuwa na mazungumzo naye.

**MAHALI SAHIHI**

Si kila mahali panafaa kwa mazungumzo mazito na muhimu. Mambo muhimu na mazito yanafaa kuzungumzwa mahali penye faragha na utulivu wa kutosha. Inashauriwa kuondoka katika mazingira ya nyumbani yaliyozoeleka na kutafuta mazingira mengine rafiki kwa ajili ya ubora wa mazungumzo.

Kisaikolojia, kubadili mazingira ni sehemu ya tiba. Wakati wa mazungumzo, simu zizimwe ili kuondoa usumbufu na mwingiliano katika mazungumzo. Ni busara kushughulika na jambo moja kwanza. Mambo mengine yaahirishwe kwa muda.

**WEKA MIPAKA YA MUDA**

Ni muhimu kukubaliana muda wa mazungumzo. Mazungumzo yasiwe mafupi sana au ya muda mrefu kutegemeana na suala linalozungumzwa. Jambo ambalo suluhu yake haijapatikana katika mazungumzo ya siku hiyo, jambo hilo linaweza kuahirishwa na mkubaliane kupanga muda mwingine wa mazungumzo.

Masuala mengine kwa sababu ya uzito wake, huhitaji muda wa ziada wa majadiliano ili kufikia suluhu. Si busara kulazimisha suluhu kwa mazungumzo ya siku moja. Mazungumzo yaliyoahirishwa yasichukue muda mrefu sana kufanyika tangu kikao cha kwanza kilipofanyika.

**ZINGATIA MADA**

Ni lazima uwe na hakika na chanzo cha mgogoro. Ni rahisi kushughulikia tatizo unalolijua kuliko shaka juu ya jambo usilolifahamu. Epuka kuzungumzia historia na kufanyia kazi mambo ya kusikia (majungu), ambayo huna hakika nayo kwa sababu aliyekuambia hujui dhamira yake.

Aidha, muhimu kujiridhisha kabla ya kuchukua hatua ili kujenga badala ya kubomoa. Wakati wa mazungumzo jikite katika tatizo la msingi unalolifahamu ili kupata ufumbuzi wake. Ni muhimu kutatua tatizo la msingi kabla ya kuzungumzia mambo mengine, kwani mambo hayo yanaweza kuwa ni matawi ya tatizo la msingi.

**Itaendelea Jumapili Ijayo**

■ ***Dk. Mlyuka ni Mchungaji wa KKKT na Mkurugenzi Mtendaji wa Tanzania Marriage and Child Care Foundation (TaMCare), asasi inayojishuhulisha na masuala ya ndoa, familia na malezi. Kwa maoni, mafunzo na ushauri wasiliana naye kwa: info@tamcare.or.tz au WhatsApp +255655865555.***

# MAISHA

FEBRUARI 14, 2021

Nipashe

Baba, Mama na Mwana

Jumapili





Ukurasa 10

**Ukiendekeza ukali kwa mtoto utamuharibu**



**MAISHA NI NYUMBA**

Kuwa mbunifu kupangilia nyumba ya nafasi ndogo



**HARUSI**

Ukurasa 12



**NGOZI LAINI**

## Mafuta ya maweze, mdalasini inatosha

Ukurasa 14

# Ukiendekeza ukali kwa mtoto utamuharibu

**Na Moses Ismail**



NI mtoto mkorofi, hasikii wala hajifunzi. Ndivyo unavyofikiria na unavyoamini kuwa ndivyo alivyo mwanao.

Kwa sababu hiyo, mara kadhaa umekuwa ukimsema na hata kumpiga makofi kila anapofanya kosa dogo. Haijalishi muwe peke yenu au iwe mbele ya wageni. Hutaki ujinga na wala si mtu wa mchezo mchezo.

Mara nyingi tu umeshamfokea na kueleza 'aibu zake' mbele ya wageni huku ukisisitiza kwa kusema; "yaani huyu ni bure kabisa. Yaani bora ningekosa mtoto kuliko kuwa na toto hili."

Ila wageni wako wamejaribu kumtetea mara kadhaa na kuwa upande wake, wamekuambia; "mbona anaonekana mtoto mpole tu." Ukasema: "Hana upole wowote, anaficha tu dhambi zao."

Ni kweli kuwa kwa tabia yake anaonekana kama mtoto mpole, ila kiuhalisia si mtoto mpole kama inavyofikiriwa, ilivyo ni kuwa hali ya upole anayoonyesha inatokana na kukosa nafasi ya kuzungumza hisia zake mbele ya wazazi wake.

Ataipata wapi wakati kila mara amekuwa ni mtoto wa kufokewa kwa kila kosa dofo afanyalo na hata akionyesha hali ya kufurahi au anapofanya jambo zuri unaishia kumwmbia; "basi leo umefanya hivyo, subiri baadaye tuone."

Kwa hisia zako mbaya kwake unategea kuwa baada ya muda fulani tu lazima atafanye kakosa, hata lie kadogo tu, halafu umshushie mananeo na 'kichapo' ili kukamilisha imani yako kuwa yeye si mtoto wa kufanya mambo mazuri.

Kwa sababu ya mapito ya malezi ya aina hiyo, anazidi kuwa mtoto mkimya mbele yako na hata kwa marafiki zako watu wazima anaofahamu kuwa wanazijua 'aibu zake' na hujawahi kusikia akikueleza hisia wala ndoto za maisha yake.

Kiujinga ujinga tu, unaamini kuwa unajua kwa nini hawezi kuzungumza 'upuuzi wake' mbele yako, unaamini kuwa hana hisia wala ndoto njema bali ni mtoto mpuuzi tu!

Lakini katika hali halisi ni kwamba ukimya huo anaoonyesha dalili kuwa mtoto wako anakumbwa na tatizo baya la ugonjwa wa sononi (depression) unaotokana na mgandamizo wa hisia mbaya za kutopendwa na wazazi wake.

Ile hali ya kumuona akipenda kukaa peke yake chumbani wakati wewe ukiwa na wenzake sebuleni mkiongea na kule kupatwa na mstuka kila anaposikia sauti yako au anapokuona, ni dalili za awali zinazoonyesha kuwa ana sononi.

Bahati mbaya ni kwamba wewe si mtaalamu wa saikolojia wala sosholojia, kwa hiyo huwezi kutambua jambo hilo na badala yake unaona kama mambo yote anayoyafanya ni dalili za kiburi kwa hiyo uanaongezea kumfokea zaidi.

Iwapo una mtoto anayeonyesha dalili hizo na umemlea kwa malezi ya aina hiyo, tambua kuwa umeshamtumbukizia kwenye tatizo kubwa na unapaswa sasa kuwaona wataalamu wa saikolojia na sosholojia ili wamrudidhe mstalini. Acha ukali usio na kipimo kwa mtoto wako.

## NA HAMIS KIDAGO 0657 207168 QUIZ

**AndikakitenziOuvrir(yaanikufungua) katikanyakatitofautikamazilivyoainishwahapochini.**

**Indicatif présent**
j' ..............
tu ..............
il/elle .............
nous................
vous ...............
ils/elles ..............

**imparfait**
j' ......................
tu ......................
il/elle ....................
nous ....................
vous ...................
ils/elles .................

**future simple**
j' ...................
tu ..................
il/elle .................
nous ................
vous ................
ils/elles .......................

**passé simple**
j' ........................
tu ........................
il/elle ........................
nous .......................
vous .....................
ils/elles ....................

**passé compose**
j' ai ...............................
tu as ..............................
il/elle a ..............................
nousavons ..............................
vousavez ..............................
ils/ellesont ..............................

**plus – que – parfait**
j' .........ouvert
tu .........ouvert
il/elle .........ouvert
nous..........ouvert
vous.........ouvert
ils/elles...........ouvert

**futurantérieur**
j' ..........ouvert
tu ..........ouvert
il/elle .........ouvert
nous .............ouvert
vous ..........ouvert
ils/elles .............ouvert

**passéantérieur**
j' eus ..............
tueus .............
il/elleeut .............
nouseûmes .............
vouseûtes ..............
ils/elleseurent ...............

**Conditionnel présent**
j' ................
tu ................
il/elle ..............
nous ..............
vous ..............
ils/elles ................


**passé**
j' aurais ..................
tuaurais ..................
il/elleaurait ..................
nousaurions ..................
vousauriez ..................
ils/ellesauraient ..................

**Infinitif présent** **passé**
.......... ......................

**Participe présent** **passé**
................ ........../....
............/tes
ayant .................

## WATOTO

# PAKA RANGI







Alichokifanya daktari

WANAFUNZI waliulizwa na mwalimu wao nani angependa kwenda peponi?

Wote wakanyoosha mikono , lakini mmoja alipokwenda nyumbani kwao akamuelezea mama yake suala hilo.

Mama yake alimuuliza, je, wewe ulinyoosha?

Mtoto akajibu "hapana"

Mama alimuuliza tena "Kwa nini"

Mtoto alijibu "Mama uliniambia nikitoka shule nije moja kwa moja mpaka nyumbani nisiende kokote"

**SWALI**

Kilimo cha chai kinapatikana wapi nchini Tanzania?

## MAISHA NDIVYO YALIVYO



Na Flora Wingia

# Je, unajua maisha yako yanaongozwa na nguvu gani?-2

KARIBU tena msomaji wangu tuendelee na mada yetu niliyoianza wiki iliyopita. Niliuliza swali kuhusu nguvu gani inayokuongoza katika maisha yako. Nilitaja 'hatia' kama moja ya eneo linalotesa watu wengi.

Hatia nilisema pamoja na mambo mengine kwamba ni ile hali ya kuendelea kuishi ukiwaza mambo yaliyowahi kukupata. Iwe ni mateso katika ndoa, kupata hasara katika biashara, chuki, hasira iliyokushika ukatenda jambo fulani baya, imani mbaya, hofu mbaya na kadhalika.

Sasa leo nijielekeze kwenye, chuki, hasira na wivu, vitu ambavyo vinaisumbua sana jamii yetu. Wapo watu wanaoongozwa na chuki, hasira katika maisha yao ya kila siku. Utaona mtu unamsemesha vizuri lakini yeye anakujibu vibaya, kumbe wala siyo wewe uliyemuudhi.

Katendewa mabaya na mtu mwingine lakini anakujibu kwa ghadhabu. Mtu wa aina hii anaongozwa na chuki na hasira. Msomaji wangu, wewe ni kitu gani kinakuongoza? Unamuuliza mfanyakazi mwenzako, "hivi bosi amesema tuandae ratiba gani ya kazi? Yeye anakujibu kwa mkato, " kwani wewe hukuwepo?". Mtu wa aina hii ana uchungu wa ndani. Anapaswa kuutoa kwa kusamehe ili awe huru.

Msomaji, elewa kuwa unapomsamehe faida ni yako. Unapokaa na uchungu, yule aliyekukosea ameshasahau. Wapo watu wa aina hiyo, anakukwaza halafu anasahau. Yeye ana amani, anacheka lakini wewe umenuna mwenzako ana furaha. Achilia ili uiponye nafsi yako.

Acha chuki na hasira za ndani. Msamehe mwenzako hata kabla hajakuomba msamaha. Siyo hadi aje akupigie magoti. Ukiachilia utaona amani ya Mungu ikijaa ndani ya moyo wako. Hata sura iliyokuwa imekunjamana, itaanza kuwa na mvuto na watu wakikuona wanaanza kukufurahia. Maisha Ndivyo Yalivyo.

Dawa la kosa ni kusamehe kwani huwa ni faida kwako wewe. Chuki siku zote huleta maumivu na pia hasara katika maisha ndani ya familia zetu. Huo ndio ukweli. Waliokuumiza zamani hawawezi kuja tena kwako, samehe na Mungu atakufurahisha.

Utashangaa neema ya Mungu ikija juu ya maisha yako. Kwa habari ya hasira neno la Mungu linasema; Ayubu 5:2 "Kwani hasira humuua mtu mpumbavu, nao wivu humuua mjinga". Magonjwa mengine unayopata ni kwa sababu ya hasira ulizo nazo. Achilia, Mungu atakuhudumia. Unapokuwa na hasira, magonjwa nayo yanakuandama.

Mtu mwenye vinyongo, moyo huugua. Kuna mioyo ya watu inaumwa kwa sababu ndani yao kuna vinyongo, hasira. Achilia na hakikisha moyo wako unakuwa mweupe, msafi usio na makunyanzi. Yeyote anayekukwaza, wewe msamehe mapema. Kama huwezi muombe Mungu akupe nguvu ya kusamehe kwani yeye ni muweza wa yote.

Ni mtu mjinga tu awezaye kusema kuwa, 'nimekusamehe lakini sitasahau'. Huyu hana maarifa kwani anafanya kitu kitakachomuangamiza yeye mwenyewe. Wengine wana makusudi, yaani amekukwaza, lakini ndio kwanza anapita mbele yako kwa maringo. Sasa unafanyaje? Mpuuze huyo naye atajiona mjinga!

Nikwambie msomaji wangu, ukisamehe unaponya moyo wako. Vituko vyake wewe vifurahie kwa sababu unajua siri ya kusamehe ambayo ni amani, furaha na utulivu. Jua ya kwamba wakwazaji wapo siku zote iwe ni mume, mke, rafiki, jirani na kadhalika.

Ukila vizuri watakusema, ukivaa nguo mpya, gumzo mtaani ili mradi tu ni wachokonozi. Yote hayo yasiharibu moyo wako. Wengi wa watu wa aina hiyo mbali na chuki, pia wamejawa na wivu usio na sababu. Wanasahau kwamba kila mbuzi hula urefu wa kamba yake.

Msomaji wangu, nimechukua muda mwingi kuelezea umuhimu wa kusamehe kwa sababu wakwazaji tunaishi nao siku zote. Na familia nyingi zimejikuta katika mitikisiko mikubwa huku ndoa zikivunjika, kusambaratika kutokana na chuki, hasira na wivu.

Ni ndoa ambazo zilikuwa na utii, kuheshimiana, amani na uvumilivu lakini msamaha haukupewa nafasi. Matokeo yake wanandoa wamekuwa maadui na mashauri ya talaka yamejaa mahakamani.

**Mpenzi msomaji, leo naishia hapa. Wiki ijayo nitajadili woga. Je, wale wanaoongozwa na woga, maisha yao yakoje? Kama una maoni, ushauri au kisa cha kimaisha unachopitia nijulishe kwa ujumbe mfupi kupitia 0715268581.**

## NAWAZA KWA SAUTI



Na Salome Kitomari

# Ya soko kuu Morogoro yako pia kwingine, yafuatiliwe

HIVI karibuni Rais John Magufuli alielekeza wafanyakazi wa manispaa na Mkoa wa Morogoro waliopangisha vibanda vya biashara katika jengo la soko kuu na kisha kupangisha wafanyabiashara kwa Sh. 20,000 hadi 50,000 kwa mwezi kurudisha fedha na vibanda hivyo, maarufu kama vizimba.

Kati ya fedha hizo inayokwenda serikalini ni Sh. 20,000 huku inayosalia ikienda kwa wachache ambao wameamua iwe hivyo na wamegeuza maeneo hayo kama mtaji wa kujipatia fedha na hilo likiwa ni jambo la kawaida katika maeneo mengi yenye vibanda vya wafanyabiashara.

Rais alieleza kusikitishwa kwake na wafanyabiashara hao wanavyoumizwa na kodi hizo kiasi cha kushindwa kufanya biashara na wengi huyakimbia majengo hayo.

Jambo hili limesababisha kuwapo urasimu kwenye kupata vibanda vya biashara katika majengo haya na mwisho wa siku waliokuwa walengwa wakiachwa nyuma na kunufaisha wachache. Jambo hilo kwa vyovyote halimnufaishi mfanyabiashara ambaye alisubiri kwa hamu maboresho ya soko au jengo la biashara.

Lakini hali hiyo pia imesababisha majengo mengi ya kisasa ya masoko yanayojengwa kukimbiwa na wafanyabiashara, sababu ikiwa wazi kabisa kuwa wanaona ni bora kurudi mtaani kama pembeni ya barabara ambako hatalipa kodi kubwa na atapata wateja kwa wingi.

Mifano hai iko katika jengo la Machinga Complex jijini Dar Es Salaam ambalo limekibiwa na wamachinga na sababu kubwa inayoelezwa ni kwa kuwa wateja hawapandi kwenye maghorofa bali wanataka kupata bidhaa eneo rahisi.

Kwa sasa serikali imetumia mabilioni ya fedha kujenga majengo ya kisasa katika masoko ya Dar es Salaam na Kituo Kikuu cha Mabasi ya mikoani Mbezi Luis, lakini kupata kibanda cha biashara katika eneo hilo ni kazi kubwa na bei zake ni kubwa.

Ukifuatilia baadhi ya majengo kabla ya kukamilika, vibanda vinakuwa vimeshajaa na vinapangishwa kwa bei kubwa ambayo mlengwa wa kawaida



hawezi kumudu, jambo ambalo ni hatari na baya kwa kuwa idadi ya wafanyabiashara wadogo waliolengwa utaendelea kuwapo mtaani.

Hili lililoibuliwa na Rais ni jambo la kweli lipo na linafanyika maeneo mengi yenye vibanda hivi na wanaoumia ni watu wa chini.

Ukifuatilia kwa nini watu wanafanya biashara katika maeneo mabaya lakini mara baada ya soko kuboreshwa wachache humudu kuingia kwenye vibanda hivyo na wengi wanajikuta nje, sababu kubwa inayoelezwa ni kukosekana kwa wateja.

Lakini sababu kubwa ni gharama kubwa isiyoendana na fedha wanazopata kutokanana kuuza bidhaa ndani ya soko, wakati huo kukiwa na gharama nyingine kama ushuru na usafi.

Ni muhimu sana uchunguzi ukafanyika kwenye maeneo yote yenye majengo ya wafanyabiashara wadogo, kwa kuwa naamini kinachowashinda ni mzigo mzito wa ushuru na kodi lakini pia ni muhimu wakafanya uchunguzi wa hali ya masoko au maeneo hayo kabla na baada ya kujengwa kisasa.


Sababu nyingine zinazoelezwa huwa ni kukosa wateja kutokana na kuibuka kwa wafanyabiashara wengine ambao huanzisha biashara kama hizo nje ya soko husika na wateja wanaona uvivu kupanda ghorofani au kwenda mbali wakati bidhaa zinapatikana nje, na wakati huo ushuru unakusanywa hadi nje bila kujali wapo kwenye vizimba sahihi au la.

Masoko haya na maeneo ya wafanyabishara yana faida nyingi ikiwamo kuongeza mapato kwa halmashauri, kuboresha afya za watumiaji yaani wauzaji na wanunuzi, kuboresha muonekano wa mji au jiji kutoka kuwa na vibanda vyenye maturubai au miavuli kwenda eneo lililopangwa vyema.

Kuwa na majengo ya kisasa yenye miundombinu muhimu kutasaidia kuboresha afya za watu na kupunguza mzigo wa matibabu kwa serikali, kwa kuwa kama masoko yako ovyo ambayo wakati mwingine hutumiwa na watoto wa baadhi ya wafanyabiashara.

Pia, afya za watu zitakuwa salama muda wote na itasaidia sana kupunguza gharama za matibabu ambazo serikali au mtu binafsi atatumia, au nguvu kazi kupungua kutokana na gharama za matibabu.

HARUSI





**Mitindo mipya ya suti inayoweza kukupa furaha kuvaa katika harusi mwaka 2021**





MITINDO

JINOGESHE ZAIDI

# Miwani na mwonekano murua



MIWANI ni moja ya pambo linalopendwa kuvaliwa na watu wa jinsia zote, ni kama kionjo cha kuongeza mvuto wa mwonekano kwa mtu husika.

Hakuna takwimu sahihi kati ya wanaume au wanawake wanaongoza kwa kuvaa miwani, lakini itoshe kueleza kuwa kuna ongezeko la watu wanaovaa miwani katika miaka ya hivi karibuni.

Kuna aina nyingi ya miwani pamoja na mitindo ambayo huwavutia watu na kisha kuingia katika uvaaji wa pambo hili.

**MIWANI YA RAY**

Miwani ya Ray inapendwa kuvaliwa sana na watu maarufu kutokana na muonekano wake wa kupendeza.

Kampuni inayozalisha miwani ya aina hii, imefanya kazi kwa kpindi cha karne, lakini kutokana na kuzalisha bidhaa nzuri watu wengi wanapenda kutumia.

Mawani aina ya 'Unisex', huvaliwa sana na wanawake na hii ni kutokana na mwonekano wake kuwa maridadi, hasa pale akivaa Jeans na shati jeupe.

**FIRM OAKLEY13**

Miwani ya jua ya Firm Oakley13, inaaminika ndiyo mizuri zaidi kutokana na muundo wake unaompa mtu uhuru wa kutazama.

Watu wanaovaa miwani ya aina hii wanakuwa na mwonekano tofauti wenye furaha na mvuto wa kipekee.

**MIWANI YA DIOR**

Ni miwani yenye mitindo ya kisasa zaidi, mara nyingi wabunifu na wanamitindo huitumia kwa ajili ya kuboresha bidhaa zao.

Hakuna shaka unapovaa miwani ya Dior unaonekana unakwenda na wakati na mwenye kujipenda.



## UREMBO



NGOZI LAINI

# Mafuta ya mawese, mdalasini inatosha

UREMBO una tafsiri pana miongoni mwa watu, wapo wanaodhani neno hilo hubeba halisi ya uzuri wa umbo na sura kwa mtu husika.





Kutokana na tafsiri hizo zisizo sahihi, baadhi ya wanawake wanajikuta wakitumia mbinu mbalimbali kama kujiongezea urembo kwa kutumia kemikali hatari ili kubadilisha muonekano wa ngozi yake.

Hata hivyo, maana halisi ya urembo ni vile jinsi mtu anavyojiweka kulinda mwili na afya yake katika muonekano ule ule. Hii ina maana kwa kutumia mazingira na vitu vinavyokuzunguka unaweza kuboresha uzuri wako bila kutumia bidhaa kutoka viwandani.

Kwa mfano, unaweza kurekebisha ngozi yako, nywele na mapambo kwa kutumia vitu vya asili pekee.

Katika nchi za kiafrika, kumekuwa na kampeni nyingi za matumizi ya matunda na miti ya asili kwa ajili ya urembo.

Je unajua kwamba, mafuta ya mawese na mdalasini yanaweza kukusaidia kukupa mwonekano bora zaidi wa ngozi yako? Kama hifahamu, basi leo utaweza kupata elimu kuhusu matumizi ya vyakula katika kukuongezea mng'aro wa ngozi yako.

**JINSI YA KUFANYA**

Chukua mafuta ya mawese nusu chupa ya soda na unga wa mdalasini ujazo wa kikombe kimoja cha chai.

Kisha changanya kwa kutumia mikono mpaka uhakikishe umepata mchanganyiko mzuri.

Weka mchanganyiko wako katika chombo maalum, tayari kwa kujipaka mwilini.

Safisha mwili wako kwa maji ya vuguvugu kwa kutumia sabuni ya kawaida kila unapotaka kutumia mchanganyiko wako

Ukimaliza jipake mchanganyiko wa mdalasini na mawese mwilini kma unavyopaka mafuta ya kawaida.

Ili kupata matokeo mazuri, tumia mchanganyiko huo kwa muda wa wiki moja, utaona mwili wako utakavyobadilika kwa kuwa na ngozi laini na yenye kung'ara.

## MAPISHI

**Na Mary Geofrey**

# Vitumbua vya nyama tamu



WATU wamezoea kula vitumbua vilivyokaangwa kutokana na unga wa mchele.

Lakini leo katika safu yetu ya mapishi , tutapeana uzoefu wa namna kupika vitumbua vya nyama ambavyo ni nadra sana kuvikuta hotelini au kwenye migahawa.

**MAHITAJI**

Nyama ya kusaga robo, kitunguu kimoja, kitunguu swaum nusu kijiko, karoti moja, pilipili hoho nusu, mayai 5 au 6.

Baking powder nusu kijiko kidogo, pilipili manga kiasi, pilipili mbichi(ukipenda) na chumvi kiasi.

**NAMNA YA KUPIKA**

Safisha nyama, iweke vitunguu swaum, chumvi, pilipili manga na tangawizi, ibandike jikoni ili iive na ikauke vizuri.

Kata vitunguu, hoho, pilipili na uvichanganye na mayai, kisha vyote vitie kwenye nyama.

Weka kwenye blender mchanyanyiko wako uusage kidogo ila usiwe laini sana. Ikiwa tayari, mimina katika bakuli.

Weka baking powder, karoti na chumvi kidogo kisha changanya vizuri, andaa chuma cha kukaangia vitumbua, bandika jikoni na weka mafuta kidogo.

Mafuta yakipata joto chota kwa upawa mchanganyiko wako utie kwenye kikaango, vikiiva upande mmoja geuza na upande wa pili uive kisha uvitoe.

Endelea kuchoma hadi viishe vyote, hapo tunakua tumemaliza pishi lako la vitumbua.

Vitumbua vyako vitakuwa tayari kwa ajili ya kuliwa na chai, soda, juisi au kinywaji kingine.

MAISHA NI NYUMBA

# Kuwa mbunifu kupangilia nyumba ya nafasi ndogo

**Na Elizabeth Zaya**

ASILIMIA kubwa ya wakazi wanaoishi mijini wanaishi katika nyumba za kupanga.

Kutokana na hali halisi ya familia za kiafrika ni chache ambazo huwa na uwezo wa kumudu kupanga nyumba nzima au kubwa ya kutosheleza familia nzima.

Kama ilivyo desturi kwa familia hizo, nyingi zinajumuisha zile kama zinavyojulikana kwa lugha ya kigeni 'extended family', hivyo familia kuwa kubwa pasipo kulingana na kipato kilichopo cha kumudu kupanga nyumba kubwa.

Kwa hiyo ili kumudu kuishi katika sehemu ndogo ya nyumba kulingana na uwezo uliopo na ukubwa wa familia iliyopo, lazima ubunifu na akili nyingi itumike katika kupangilia vitu ili nafasi katika nyumba hiyo itosheleze mahitaji.

Pia kuna haja ya kupunguza kuweka ndani ya nyumba baadhi ya vitu visivyo vya lazima.

Kwa upande wa uwekaji wa fanicha katika nyumba hiyo ndogo ni lazima uhakikishe kwamba unaweka zenye umbo dogo na ambazo zitakuwa na sehemu ya kuhifadhia vitu vingine au zenye matumizi zaidi ya moja.

Kwa mfano meza ya televisheni, unaweza kuweka ambayo inakuwa na matumizi ya kuwekea TV na pia kwa kuhifadhia vitu vingine hususani vitabu na kadhalika.

Tumia sehemu ya ukuta wako wa dari 'kudizaini' kwa ajili ya kuwekea vitu vingine kama mapambo na kama ni jikoni unaweza kujengea na kuweka vyombo na vitu vingine na likatumika kama kabati la kawaida la vyombo.

Kabla ya kutengeneza fanicha hizo, hakikisha kwanza umepima nafasi iliyopo na ni muhimu kuzingatia zaidi upangaji wa vitu vyako ndani uwe wa kutumia hesabu zaidi siyo kuweka ilimradi.

Epuka kuweka vitu ovyo ikiwezekana panga ambavyo una uhakika ni vya muhimu zaidi.

Kwa upande wa viti au sofa, hakikisha unaweka ambazo hazichukui nafasi kubwa, kabla ya kununua au kutengeneza ni vema ukapima nafasi ambayo umepanga kuziweka.

Tumia ubunifu katika sehemu za kona za nyumba yako kuweka fenicha zako, hususani meza na televisheni na uhakikishe nazo zinakuwa ni zile ambazo hazichukui nafasi kubwa na ikiwezekana ziwe ni nyembamba zenye nafasi ya kuelekea juu na si kwa upana.

Usiweke kitu ilimradi umeona kwa jirani yako ameweka, isipokuwa kwa kuzingatia umuhimu wake, na nafasi uliyonayo kwenye nyumba yako.

Pia katika siku za hivi karibuni kwa upande wa fanicha, kumekuwapo mabadiliko makubwa, pesa yako ndiyo inaweza kuamua uwe nayo ya dizaini gani.



MPANGILIO

## Dondoo muhimu namna ya kuchagua Wallpaper ndani ya nyumba yako

**1:** Zingatia kiasi cha mwanga kwenye chumba husika ili kujua kama inafaa wallpaper ya rangi nzito au nyepesi.


**2:** Zingatia ukuta wa chumba chako kama cha kulala au sebuleni ili kupata aina ya wallpapaer zinazofaa. Kama chumbani zenye maua nzuri zaini na sebuleni yenye mapambo ya mtindo wa kisasa inafaa.

**3:** Chagua mitindo mizuri ya kubandika wallpaper, aina nyingine hazileti muonekano mzuri.

**4:** Ukubwa wa chumba ni muhimu sana, chumba kidogo kinapendeza wallpaper isiyo na michoro au maua na kikubwa kinapendeza kwa wallpaper yenye michoro na maua makubwa.



# KATUNI




*KINYUNYIZO CHA LEO...

## HABARI KIMATAIFA

# Viongozi 15 wakamatwa kwa ufisadi mazishi ya Mandela

**PRETORIA, Afrika Kusini**

WATU 15 wamekamatwa nchini Afrika Kusini wakikabiliwa na mashtaka ya wizi na ulaghai katika maandalizi ya mazishi ya rais wa zamani Nelson Mandela mwaka 2013.

Watu wanaohusishwa katika tuhuma hiyo ni wanachama maarufu wa chama tawala cha African National Congress (ANC) katika jimbo la Eastern Cape.

Serikali wala chama tawala bado hawajasema lolote kuhusiana na tuhuma hizo.

Waendesha mashtaka wanawashutumu kwa vitendo vya ufisadi na utakatishaji wa pesa takriban dola 700,000.

Mandela alikuwa ni rais wa kwanza mweusi baada ya utawala wa ubaguzi wa rangi mwaka 1994.

Tuhuma zilitolewa kwa mara ya kwanza mwaka 2014, miezi kadhaa baada ya kumalizika mazishi ya Mandela yaliyofanyika katika kijiji cha Qunu, Eastern Cape, Septemba, mwaka 2013, na kuhudhuriwa na wakuu wa nchi mbalimbali duniani.

Wanaokabiliwa na mashitaka hayo ni Waziri wa afya wa jimbo la Eastern Cape , Sindiswa Gomba, wafanyabiashara maarufu na wabunge wengine kutoka chama tawala cha ANC.

Pia wanaoshikiliwa ni mwenyekiti Pumlani Mkolo, meya wa zamani wa jiji la Buffalo City, Zukiswa Ncitha na Spika wa Baraza la chama hicho, Luleka Simon-Ndzele.

Waendesha mashtaka wanadai kuwa walitoa madai ya ulaghai kuhusiana na usafirishaji wa waombolezaji na eneo lililotumiwa katika mji wa mashariki mwa London kwa ajili ya ibada za maombolezo ya kifo cha Mandela.

Hata hivyo, viongozi hao walipewa dhamana na wanatarajiwa kufika mahakamani tarehe 5, Machi mwaka huu. **BBC.**



Mwendesha mashitaka mpya wa Mahakama ya Kimataifa ya Uhalifu wa Kivita (ICC), Karim Khan. **(PICHA: DW)**

# Khan mwendesha mashtaka mpya ICC

**NEWYORK, Marekani**

MWANASHERIA wa Uingereza, Karim Khan, amechaguliwa kuwa mwendesha mashtaka mpya wa Mahakama ya Kimataifa ya Uhalifu (ICC), akichukuwa nafasi ya Fatou Bensouda, ambaye anamaliza muda wake wa miaka 9 mwezi Juni.

Khan alichaguliwa katika kura ya pili ya siri na wanachama 123 waliotia saini mkataba wa Roma ulioanzisha mahakama hiyo.

Mwanasheria huyo ambaye amejikita katika sheria ya kimataifa na haki za binadamu, alipewa nafasi kubwa ya kushinda kura hiyo.

Hata hivyo, katika duru za mwanzo hakuna mgombea aliepata uungwaji mkono wa kutosha ili kuteuliwa moja kwa moja na kusababisha kurudiwa kwa upigaji kura siku ya Ijumaa katika ukumbi wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa.

Makamu wa Rais wa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa, Michal Mlynar, alimtangaza Khan mshindi baada ya kumalizika upigaji kura.

Khan alipata kura 72, aliyemfuatia alikuwa Fergal Gaynor kutoka Ireland, kwa kura 42, na Mhispania Carlos Castresana Fernandez, alishika nafasi ya tatu kwa kura tano.

Kabla ya kuchaguliwa, Khan alikuwa akiongoza timu ya Umoja wa Mataifa iliyoundwa kwa ajili ya kuchunguza madai ya mauaji ya kimbari, uhalifu dhidi ya ubinadamu na uhalifu wa kivita vilivyotendekea na kundi la Dola la Kiislamu nchini Iraq.

Amefanya kazi kama mwendesha mashtaka wa mahakama inayoshughulikia uhalifu wa kivita katika Yugoslavia ya zamani, na uhalifu dhidi ya ubinadamu na mauaji ya kimbari nchini Rwanda.

**DW**

# Gereza la Guantanamo Bay kufungwa

**WASHINGTON, Marekani**

RAIS wa Marekani, Joe Biden, amewekwa nia ya kulifunga gereza la Guantanamo Bay, lilopo nchini Cuba ambalo linatumiwa kuwashikilia washukiwa wa ugaidi kabla ya kumaliza muhula wake.

Msemaji wa Ikulu ya White House, Jen Psaki, alisema hayo wakati alipozungumza na waandishi habari.

Gereza hilo la kijeshi lina wafungwa wanaohusishwa na kile kinachoitwa na Marekani kama vita dhidi ya ugaidi, akiwemo Khaled Sheikh Mohammed raia wa Pakistan, ambaye alitangaza kuwa ndiye mkuu wa mashambulizi ya Septemba 11, mwaka 2001.

Hadi sasa gereza hilo bado lina wafungwa karibu 40 hadi 26 miongoni mwao wanaochukuliwa kuwa ni hatari iwapo wataachiwa huru

**DW.**

============================ ===

# Watatu wauawa Somalia

**MOGADISHU, Somalia**

WATU watatu wameuawa baada ya bomu kulipuka karibu na kituo cha ukaguzi nchini Somalia.

Bomu hilo lilikuwa limetegwa ndani ya gari, lilipuka katika barabara kuu ya mjini Mogadishu.

Ofisa wa usalama, Abdirahman Mohamed, alisema polisi walikuwa wakilikimbiza gari hilo baada ya kuliona likiwa umbali wa kilomita chache kutoka mahali lilipolipuka. Hatua hiyo, alisema kitendo hicho kiliwapa fursa watu kukimbia na kupunguza idadi ya vifo na majeruhi. Wanamgambo wa kundi la al-Shabab, wamekuwa na kawaida ya kuushambulia kwa mabomu mji wa Mogadishu kwa muda mrefu.

**DW**

# Tatizo si mfumo wa Elimu



Na Magabilo Masambu

KUMEKUWAPO na mjadala kuhusu mfumo wetu wa elimu. Tulio wengi tunasema mfumo wetu wa elimu ni mbovu ndiyo maana vijana wengi wanamaliza vyuo vikuu lakini hawawezi kujiajiri. Kelele ziko kila kona ya nchi.

Malalamiko haya hayatoki kwa wananchi wa kawaida tu bali mpaka wenye nafasi ya kufanya uamuzi. Katika mjadala wa bunge hivi majuzi, hoja hii pia ikaonekana kujadiliwa katika hali ya kulalamika.Waswahili husema lisemwalo lipo kama halipo laja, inawezekana lina ukweli ndani yake.

Kwa maoni yangu, tunajaribu kutafuta dawa kwa tatizo lisilo lenyewe. Ninachokiona si ubovu wa mfumo wa elimu bali ni ufinyu wa fursa za ajira kwa sababu si kila aliyejiajiri alipata elimu bora. Kuna watu shule hawaijui kabisa lakini wamejiajiri.Tujiulize maswali machache hapa.

Je, tunataka kusema nchi hii haina wataalamu katika maeneo mbalimbali, madaktari na wauguzi, walimu, wahandisi, wahasibu, marubani, manahodha, wanasheria, mafundi umeme, wataalamu wa miamba na kadhalika? Kama wapo walipata elimu yao katika mfumo gani? Walisoma katika nchi gani? Walifundishwa na kina nani? Viongozi wetu kuanzia rais wamesoma wapi? Tuna maprofesa ndiyo kusema nao ni matokeo ya mfumo mbovu kwa hiyo nao ni wabovu?

Bila shaka jibu ni kwamba wamesoma Tanzania na mfumo wetu wa elimu haujawahi kubadilika ni ul eule wa mzungu. Je, ni kweli hawafai? Kama wanafaa hawa wengine kwa nini waonekane wamepata elimu mbovu? Maswali ni mengi kuliko majibu.

Tukikubaliana kwamba mfumo wetu wa elimu ni mbovu kiasi hicho, maana yake hata wale tunaolalamika vilevile tulipata elimu mbovu, pengine ndiyo maana tunashindwa kutengeneza fursa za ajira kwa vijana wetu. Tumeshindwa kujiajiri ila tunataka vijana wajiajiri!

Tukubaliane tu kwamba tatizo la ajira ni la kidunia kwa sababu ya ongezeko la watu. Jambo la msingi ni kufikiri njia sahihi ya kutengeneza ajira katika maeneo mbalimbali hasa kwenye kilimo badala ya kuwanyanyapaa vijana wetu ambao wamehitimu elimu tunayoisimamia. Yaani ni sawa na wazazi kumlaumu mtoto wao kwa kuzaliwa wakati wao ndiyo walitaka azaliwe.

Vijana wanaohitimu ngazi mbalimbali za elimu nchini si wapangaji wa mfumo wa elimu. Tunapowalaumu kwamba hawawezi kujiajiri, tunawakosea sana wao ni zao la mfumo huo wa elimu kama ni mbovu. Tusiwaongezee majonzi, tusiwasakame tukifanya hivyo tunaweza kujikuta tunaongeza idadi ya vijana watakaokuwa wanatembea barabarani wakiongea wenyewe au hata kuwasababishia vifo vya kujinyonga kwa kukosa matumaini ya kuishi bila kazi.

Tumekazania sana kufaulisha shule za msingi na sekondari ili waende kwenye vyuo mbalimbali lakini nafikiri hatujafikiria zaidi mahali gani watakwenda baada ya kuhitimu vyuo. Kama tumeshagundua tatizo kwanini tuendelee kulalamika bila kuchukua hatua za kubadili mfumo wa elimu kama ni mbovu?

Tanzania hatujawa na viwanda vya kusema kila mtu anaweza kupata ajira lakini tuna ardhi kubwa, tunayo maji ya kutosha, Ziwa Victoria, Nyasa, Tanganyika, Rukwa, Manyara na na kadhalika. Pia tunayo mito ya kutosha. Juhudi gani zimechukuliwa kuhakikisha fursa hizi za ardhi na vyanzo vya maji vinakuwa ajira?

Kwa idadi yetu sasa ni wazi kwamba serikali haiwezi tena kuajiri kila mtu, kwahiyo ni busara kuweka mazingira rafiki katika sekta binafsi, ili ziweze kusaidiana na serikali kuajiri au kutengeneza fursa za vijana kujiajiri. Uhakika nilio nao ni kwamba hata kama kila mtu akaamua kusoma elimu ya ufundi au kazi za mikono ambazo wengi wanasema zitakuwa mkombozi, bado halitakuwa jambo rahisi kujiajiri kwa sababu hakuna namna bora ya kutafuta masoko ya bidhaa zitakazotokana na kazi hizo.

Ushauri wangu ni kwamba Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana na Ajira; Wizara ya Kilimo, na Wizara ya Viwanda na Biashara ni muhimu kukaa pamoja ili kutafuta majawabu ya namna ya kutengeneza fursa za ajira kwa kushirikiana na sekta binafsi.

Tunaweza kuamua maeneo yote ya Kanda ya Ziwa na mito yakawa maeneo ya kuzalisha vyakula vya aina zote na kazi hiyo ikafanywa na vijana kwa kufanya kilimo cha umwagiliaji. Wanaweza kuuza vyakula hivyo ndani na nje ya nchi wakatafutiwa masoko ya uhakika.

***0689157789***
***magabilomjalifu@gmail.com***
***ARUSHA-TANZANIA***

# Wali wa kupalia mkaa umekwenda na 'rice cooker'



Na Adam Fungamwango

KWENYE safu yetu ya 'Burudani Iliyotikisa', leo tunajikita kwenye masuala ya teknolojia na chakula.

Huko nyuma tuliwahi kuelezea teknolojia ilivyorahisisha kizazi cha sasa kupata wapenzi kwa urahisi tofauti na zamani kulivyokuwa hakuna simu za mkononi kiasi kwamba watu waliganda sana kwenye vituo vya basi, au sehemu walizoahidiana wapenzi.

Na kule vijijini ilikuwa tafrani tupu kwani watu waligandishwa kwenye miti, vichaka, huku wakiwa hawana uhakika wa wapenzi wao kuja kwa kuwa tu hakukuwa na mawasiliano. Vile visa vilivyokuwa vikitokea kutokana na kutokuwa na teknolojia ilikuwa burudani tosha.

Leo tutaingia kwenye masuala ya 'misosi'. Kwa wale waliokuwa watoto au vijana miaka ya nyuma, kabla ya mwanzoni mwa miaka ya 2000, watakumbuka kuwa kinamama wa wakati huo walikuwa wakipika wali kwa kutumia mkaa, vifuu au kuni.

Baada ya kuiva, sufuria la watu linafunikwa juu. Ule moto wa mkaa, kuni au vifuu unagawanywa. Nusu unabakishwa kwenye jiko au mafiga, halafu mwingine unawekwa juu ya mfuniko.

Kwa lugha rahisi iliyokuwa inatumika wakati ule na nadhani hata sasa ni kupalilia.

Baada ya hapo utaachwa hapo nadhani baada ya masaa mawili hivi, utapakuliwa, tayari kwa ajili ya chakula cha familia.

Wali huo utiwe na nazi au mafuta ulikuwa unanukia vizuri kwa sababu tayari juu wali unakuwa umeungua na kutengeneza kitu kama utandu na jina lake linaitwa matandu. Wengine huita mahaba ili mradi kila mtu na jina lake. Upishi wa aina hiyo ulitengeneza matandu, halafu chini ukatengeneza kitu kinaitwa ukoko.

Matandu na ukoko vilikuwa kipenzi cha watoto wa zamani. Wengi wao walipenda mno wali na maharage. Wenyewe waliita ubwabwa na maharage. Watoto wa zamani hawakuwa na makuu. Hawakuhitaji wali kuku, wali nyama, wali samaki wala nini. Wao ni wali na maharage tu. Sasa ndiyo ikute wali ulioungwa na nazi umepaliwa na maharage nayo yaungwe na nazi. Ni burudani tupu.

Sasa burudani inaanza pale kinamama wanapoanza kupika wali huo. Watoto siku hiyo hawaendi kucheza mbali. Ikumbukwe kuna miaka hasa mwishoni mwa 1970 hadi 1980, mchele ulikuwa adimu sana nchini Tanzania. Siku ikipikwa nyumbani, balaa lake linakuwa kubwa.

Wengine wanajifanya wanasinzia ili upakuliwe mapema, lakini wakishakula wanaenda kucheza. Hakuna tena usingizi. Wengine hata wale ambao ni wabishi kuoga, siku hiyo bila fimbo wala kulazimishwa wanaoga mapema. Kisa siku hiyo unapikwa ubwabwa nyumbani.

Mama atapalia na wakati wa kupakua, watoto wataanza kupewa matandu kwanza, kabla ya ubwabwa. Halafu kesho yake asubuhi, watoto huamka mapema hata kama si siku za kwenda shule. Kisa ni kwamba wanakumbuka kuwa jana ulipikwa ubwabwa, lengo ni kutaka wapakuliwe ukoko ambao unamiminiwa na maharage.

Hapo watoto wataanza kula ukoko kwanza, kabla ya kula ubwabwa na chai asubuhi. Ukimwuliza mtoto yoyote wa miaka hiyo, atakwambia utamu wa matandu na ukoko, jinsi mapishi ya kinamama wa wakati huo kutokana na kupika kwa kutumia mkaa, kuni na hata vifuu.

Kutokana na kukua kwa teknolojia, hivi sasa kwa asilimia 90 hasa maeneo ya mijini, hawatumii sana mkaa, vifuu wala kuni. Ahueni iko vijijini ambako bado kuna kuni ambazo wanatumia. Lakini pia wanawake wengi kwa sasa wamekuwa hawatumii tena aina ya mapishi ya kupalia wali, labda wale wa mikoa ya Pwani kama vile Tanga, Lindi na Pwani yenyewe hasa Bagamoyo.

Ni aghalabu sana leo kukuta wali unapaliliwa kutokana na teknolojia kwani sasa wengi wanatumia 'rice cooker' na hata jiko la gesi kupika wali, hivyo haiwezekani. Ukipika kwa njia hiyo huwezi kupata matandu wala ukoko chini. Ndiyo maana wengi waliozungumzia hili ambao ni watu wazima, walionekana kukumbuka sana matandu na ukoko, lakini kwa sasa wakadai hawawezi kuupata kwa sababu wake zao ni wa kisasa na wanatumia majiko ya kisasa.

Wengi walikuwa wanakula matandu na ukoko kwa mapishi waliokuwa wakipika mama zao enzi hizo. Kwa sasa wanabaki na kumbukumbu tu na kuzimulia kama burudani iliyotikisa, lakini ni nadra sana kuupata wali wa kupaliliwa, ambao ulikuwa mtamu na wenye kunukia.

Watoto wa kizazi cha sasa wao ndiyo kabisa. Wao ni wali wa kwenye 'rice cooker' na jiko la gesi tu. Ukimwambia mambo ya wali wa kupaliliwa, matandu na ukoko, atakushangaa tu.

# HADITHI

MILIO mitatu ya risasi ilisikika maeneo ya Keko Bora jijini Dar es Salaam. Sauti hizo za risassi ziliwafanya watu kutimua mbio na kutafuta chaka la kujificha. Kila mmoja alidhani ni majambazi waliovamia kwa ajili ya kupora pesa dukani au kwenye vibanda vya mawakala wa kampuni za simu.

Haikuwa hivyo. Aliyedhaniwa kuwa ni jambazi alichofanya ni kumpora mwanamke mtoto mwenye umri wa mwaka mmoja tu na kuondoka naye akiwa kwenye gari aina ya Toyota IST. Huyu jamaa aliyefanya hivyo ni nani? Ni kwa nini aliyemteka mtoto? Mtoto ni wa nani? Mwanamke aliyeporwa mtoto anamfahamu mporaji?

Fuatilia kisa hiki kitamu, cha kusisimua na kuhuzunisha.

# Nina Jambo Langu-9

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

"Hapana kuna vitu nataka nichukue hapa. Ila Jerry kuna kitu kinanisumbua sana, naomba ushauri wako."

"Kitu gani hicho mpenzi?"

"Basi tu. Mimi sitaki kukwambia hapa. Ni hadithi ndefu sana na hapa tutachelewa. Leo si Jumapili? Kama utakuwa na muda Jumanne njoo hapa hapa, nikuchukue nikupeleke nyumbani. Nyumbani kwa mjomba wangu. Hakuna tatizo wala usiogope, mimi ni mkubwa, nimeshaolewa nimezaa, kuna nani tena anaweza kunichunga?"

Bado Ester alikuwa akiongea na Jerry akiwa ndani ya gari, lakini likiwa limesimama akiwa anajiandaa kuteremka.

"Jambo lenyewe ni hili la jamaa aliyekutelekeza au kuna jingine jipya?"

"Usiwe na haraka Jerry, tutaongea vizuri, halafu wewe najua utanishauri vizuri ili limalizike, maana limenichosha. Limenikinahi kweli mpenzi."

"Sawa, mimi nimekuelewa, nimeamua kukusaidia kwa hilo, kama ni ushauri mimi niko tayari. Nitakuja hapa Jumanne."

"Nitashukuru sana." Ester aliteremka kwa madaha ndani ya gari. Kabla hajafunga mlango alimbusu Jerry shavuni huku baadhi ya watu waliokuwa pembeni ya barabara wakiwa mashuhuda.

"Ahsante uwe ya siku njema." Jerry alijibu baada ya kupigwa busu mwanana.

Akiwa anarejea nyumbani baada ya kuachana na mwanamke huyo, Jerry alikuwa na mawazo tele kichwani.

Aliona kabisa kuwa nafasi yake kwa Ester bado ipo.

Aliona dalili zote kuwa Ester anahitaji warudiane. Tatizo ni kwamba tayari alikuwa ameshalihamisha penzi kutoka kwake baada ya kuachana miaka mingi.

Penzi lake kwa sasa limetua kwa Neema. Neema ambaye ni mke wa mtu. Neema ambaye anajua kabisa kuwa hawezi si tu kuwa mke wake, lakini hata kuwa mpenzi wake.

Siku zote penzi ni kizungumkuti. Penzi ni kitu cha ajabu sana. Anayekupenda wewe humpendi. Unayempenda ana mwingine. Hakujua afanyeje.

Faraja yake pekee aliyoipata ni wanawake wao wote wawili, kulia mbele yake. Kila moja alimuona wa thamani kwake. Kila mmoja akitaka msaada kutoka kwake. Hakujua mwisho wa yote nini kitatokea.




Ni wiki moja imepita tangu Jerry alipokwenda nyumbani kwa Ester. Tangu huko alionekana ni mtu mwenye mawazo. Habari nzima aliyoambiwa na Ester ilimshangaza, kumsikitisha na kutisha kwa wakati mmoja.

Kikubwa zaidi ni kwamba Ester alimwomba ushauri wake kutokana na matatizo na mambo yaliyomkuta na aliyoyafanya. Hakuwa na jipya. Ni lile lile la kuolewa na kutelekezwa na mwanamume akiwa na mtoto mdogo.

Ni lile lile alilomwambia siku ya kwanza kuwa mumewe aliondoka nyumbani kwake na kwenda kuoa mwanamke mwingine. Yale ya mwisho aliyomwambia ndiyo yaliyomshangaza na kumtisha Jerry.

Alimwomba Ester ampe wiki moja ili afikirie na kuamua wazo ambalo litakuwa na manufaa kwa mlengwa. Wazo ambalo halitasababisha baadaye mtu ajute. Anashukuru Ester alimkubalia.

Kilichomshangaza zaidi ni jinsi Ester alivyomwamini na kumwambia jambo lile na kumtaka awe mshauri wake.

"Labda kwa kuwa nilikuwa mpenzi wake tangu tupo chuo." Aliwaza.

Pia alitambua kuwa mwanamke anapopenda wakati mwingine hujisahau na kuongea mambo ambayo ni siri.

Wakati akiwaza ya Ester, akili yake ikahama, ikawa inamuwaza Neema. Naye pia kuna kitu ambacho amejitolea kumsaidia. Na baada ya kujitolea, pia akaombwa kusaidia.

Sasa ni wanawake wawili wote ambao wamemwomba awasaidie. Inaelekea mwezi sasa Neema anahangaika kutafuta mtoto wake ambaye alitekwa na mtu asiyejulikana maeneo ya kituo cha Keko Bora, akiwa na mumewe. Tena walikuwa wanampeleka hospitalini.

Mpaka sasa hakuna taarifa yoyote alipo mtoto wake mtu yoyote aliyepiga simu walau tu kutaka apatiwe pesa ili amrudishe mtoto.

Ndoa ya Neema nayo iko matatani kutokana na kutekwa kwa mtoto huyo. Pamoja na kwamba yuko kwenye simanzi ya kutoelewa mtoto yu wapi? Yuko hai au amekufa? Na kama yuko hai yupo kwenye hali gani? Na aliyemteka alikuwa na dhamira gani? Yote hayo yaliyo kichwani kwake, mumewe Ben na familia yake wanahiki kuwa huenda aliyemteka mtoto atakuwa alikuwa hawara wa mwanamke huyo na amefanya hivyo, huenda anadai ni mtoto wake.

Hiyo inachagizwa zaidi na kuongelewa sana kwenye kikao chao cha familia kwa sababu kama ingekuwa ni pesa, basi mtekaji au watekaji wangekuwa wameshapiga simu kutaka mzigo. Hili nalo lilimtesa Neema.

Jerry, ambaye alipambana kwa kulifukuza gari lililomteka mtoto huyo hadi lilipoingia kwenye eneo la Ubungo Maziwa, ndiye angalau aliyemwita Neema na kumpa mwanga. Lakini wakashauriana wasimwambie mtu yoyote yule hadi pale watakapojua nini la kufanya.

Alichoamuamua ni kunyanyua simu yake na kumpigia Neema kama anaweza kufika nyumbani kwake, majira saa 10:00 jioni.

"Kwa sababu nimetoka nyumbani niko kwa shangazi, nikitoka huko nitapitia huko moja kwa moja." Alijibu Neema.

Alipomaliza kumpigia Neema, akabonyeza namba za Ester akamwomba kama anaweza kufika nyumbani kwake Chang'ombe muda ya saa 10:00 jioni.

"Nimeshatoka kazini, nitateremkia hapo Chang'ombe, nitakuwa hapo baadaye.

*************************

Majira ya saa 10:30 jioni, nyumbani kwa Jerry kulijaa wanawake wawili warembo ambao waliipamba nyumba yake.

Alikuwa amekaa katikati ya kochi la watu watatu, huku mwanamke mmoja akiwa kulia kwake na mwingine kushoto. Hawakuwa wanafahamiana. Kila mmoja alidhani labda ni mpenzi wa Jerry.

". Kutana na Ester hapa." Jerry alianza utambulisho. "Huyu ni rafiki yangu, alikuwa mpenzi wangu wakati tuku chuo, lakini alihama na hatukuonana tena. Milima haikutani binadamu wanakutana. Tumebahatika kuonana wiki mbili zilizopita maeneo ya Mtoni. Inawezekana kabisa saa hizi angekuwa mke wangu. Lakini ndiyo basi tena. Ameolewa." Alipoongea neno la mwisho, alimtazama Ester ambaye aliona anaangalia chini.

"Ester. Huyu ni rafiki yangu pia. Anaitwa Neema. Huyu nilikutana naye Makumbusho, nikampenda na nikawa nimeweka dhamira nimuoe. Lakini sikujua kumbe amesholewa na ana mtoto mmoja kama wewe." Jerry aliendelea na utambulisho.

"Pamoja na kuwa ameolewa, bado ameendelea kuwa rafiki yangu wa kawaida tu na tunasaidiana kwenye shida na raha. Kwa hiyo hapa nina wanawake wawili ambao kwangu tena si riziki yangu." Alisema na kuwatazama kwa zamu. Walionekana kuwa na hamu ya kutaka kujua kinachoendelea.

Kila mmoja alitaraji kuna cha ziada. Hawakudhani kama Jerry aliwaita kwa ajili ya kuwafahamisha kuwa mmoja alikuwa mpenzi wake na mwingine alitaka kumuoa, lakini kumbe ni mke mtu.

"Nilichowaita hapa wote wawili ni kwamba kila mmoja alinieleza matatizo yake kwa nyakati tofauti. Na nyinyi hapa kila mmoja akataka nimsaidie. Na kweli nimeamua niwasaidie. Kwa uchunguzi nilioufanya nimegundua kuwa kesi yenu inafanana. Neema na Ester matatizo yenu ni hayo hayo.

Kwa maana hiyo, nyinyi wenyewe mnatakiwa muongee, myajenge na myamalize.

Kwa mara ya kwanza Neema na Ester walitazamana usoni. Kila mmoja akiwa anataka kupata picha ya mwenzake na kwa nini matatizo yao yanafanana. Kila mmoja ana shida yake ambayo anaamini ni kubwa mno na ngumu kutatulika kwa hali ya kawaida. Leo Jerry anasema tatizo lao ni moja tu.

"Mimi nitakuwa nawapa ushauri nini cha kufanya na kuwaweka sawa, lakini ninyi hapa wanawake wawili mkizungumza vizuri, kila mmoja tatizo lake litakuwa limetatulika au kumalizika kabisa."

INAENDELEA JUMAPILI



RAHA YA MAHABA

# HARMONIZE, KAJALA WAJIACHIA

HAKUNA siri tena, ni wazi mkali wa muziki wa Bongo Fleva na mmiliki wa lebo wa Konde Gang, Harmonize, amejiweka kimahaba kwa mwigizaji Kajala Masanja.

Uhusiano wao ambao ulikuwa gumzo kutokana na kuwa siri, wawili hao wameamua kuweka wazi baada ya kusambaa kwa picha ikiwaonyesha wakila raha kisiwani Zanzibar.

Aidha kupitia posti ambazo ameshiriki Harmonize, ameandika “Karibu kwenye United State Of Konde Gang” Konde Biden na Kajala Kamala, naahidi kuwa kwa ajili”.

Katika penzi lao jipya, kila mmoja ana mtoto kutoka kwa mzazi tofauti, Kajala mtoto wake kike ‘Paulah Kajala’ alizaa na prodyuza wa muziki P Funk Majani, na Harmonize mtoto wake wa kike amempata na mzazi mwenza Shantel.

## Nay wa Mitego hachoki kulianzisha

RAPA mtukutu Nay wa Mitego, anataka kulianzisha tena, safari hii anamchokoza Harmonize, baada ya kumuuliza kama bado ana penzi na mke wake Sarah.

Kupitia ukurasa wa Instagram, Nay amechapisha picha ya Sarah, kisha aliandika ujumbe akiuliza kama mwanamke huyo yupo ‘singo’ ili usitokee ugomvi kati yake na Harmonize yeye akijisogeza.

“Kwahiyo ndio kusema yupo single si ndio, baadae isije ooh umemchukulia mwenzio, na Valentine hii yupo mwenyewe, wahuni tunaulizaga kwanza maana hatutaki zengwe akaja kupigwa mtu bure” ameandika Nay.



## We King Sure kamwambie mwenyewe

WAKATI dunia inasherehekea siku ya wapendanao leo, msanii wa muziki wa Bongo Fleva, King Sure, anatamani angekuwa karibu na staa wa BongoMovie Irene Uwoya ili kuwa na furaha zaidi.

King Sure amesema anampenda sana Irene Uwoya na tayari ameshamtumia ujumbe za kumueleza jinsi anavyojisikia, lakini hajajibiwa.

“Nampenda sana Irene Uwoya na moyo wangu pale ndiyo umekufa, nimemtumia ‘message’ kama 8 za kumuelezea hisia zangu jinsi ninavyoumia moyoni, nikiwa naye naamini kabisa hawezi kuniacha na hawezi kuwa na mwanamume yeyote kwa sababu hao wengine wanampapasa tu” amesema King Sure.



# HABARI MICHEZO

## Simeone: Tutacheza popote UEFA

**MADRID,** Hispania

DIEGO Simeone amesisitiza hana "tatizo" na mchezo wa Atletico Madrid wa Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Chelsea baada ya kuhamishiwa Bucharest.

Mchezo wa kwanza wa hatua ya 16 utachezwa katika dimba la Arena Nationala Februari 23, mwaka huu kutokana na sheria na masharti ya mlipuko wa virusi vya corona, umehamishiwa huko.

Kocha Mkuu wa Atletico, Simeone yeye amesema hawezi kulaumu hilo kwamba timu yake ameiandaa kucheza popote.

"Sidhani kama kuna umuhimu wa kutoka mawazo, kwa sababu mawazo tutakayotoa hayatakuwa na athari yoyote kutokana na ukweli ulivyo.

"Na kutokana na hilo, sisi tupo tayari kucheza popote, kwani tayari ni kazi ngumu kushindana na kufanya kazi yetu," alisema akiwaambia waandishi wa habari.

"Tutajiandaa kufurahia kucheza. Kucheza popote, muda wowote na siku wanayotaka wao.

"Hakuna tatizo na hilo."

Atletico wanaongoza kwa pointi tano kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu Hispania, LaLiga, na wana michezo miwili mkononi dhidi ya wanaoshika nafasi ya pili na wapinzani wao Real Madrid.

Hawajafungwa katika mechi zao 20 za LaLiga zilizopita (wameshinda mechi 15 na kutoka sare tano).



## BAYERN SASA KUMKOSA GNABRY



**MUNICH,** Ujerumani

SERGE Gnabry anajiandaa kukaa nje ya dimba baada ya kupata jeraha la misuli katika paja lake la mguu wa kushoto, Bayern Munich imethibitisha.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ujerumani alitolewa nje dakika ya 64 ya mchezo katika fainali ya Klabu Bingwa ya Dunia, ambapo Bayern Munich iliibuka na ushindi wa bao 1-0 na kuwa mabingwa wapya wa mashindano hayo.

Mabingwa hao wa Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, hawajaweka wazi ni kwa muda gani mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25 atakaa nje ya dimba ambapo pia walikuwa bila Thomas Muller ambaye alikutwa na maambukizi ya virusi vya corona.

Taarifa rasmi ya klabu ilisomeka: "Kwa muda uliopo Bayern watakuwa bila Serge Gnabry.

"Mshambuliaji wetu amepata jeraha la misuli katika paja lake la mguu wa kushoto kwenye fainali ya Klabu Bingwa ya Dunia dhidi ya Tigres. Haya yalikuwa ni majibu ya vipimo viliyofanywa na idara ya matibabu ya Bayern Munich."

Baada ya kushinda kombe hilo, Bayern watarudi dimbani kuchuana na Arminia Bielefeld kesho Jumatatu wakiwa nyumbani kwenye mchezo wa Bundesliga.

Baada ya mchezo huo watakutana na Lazio katika mechi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya 16 bora Februari 23, mwaka huu kabla ya kuivaa Borussia Dortmund baadaye mwezi ujao.

## *Musa ashindwa kusajiliwa West Brom*

**LONDON,** England

KLABU ya West Brom Albion imeachana na mpango wa kumsajili aliyewahi kuwa mchezaji wa Leicester City na nyota wa Timu ya Taifa ya Nigeria, Ahmed Musa.

Imeripotiwa kuwa Musa alichelewa kuwasili klabuni hapo kutokana na taratibu za kujilinda na virusi vya corona, ambapo alikuta klabu hiyo imeshawasajili wachezaji wengine wanne.

Katika usajili wa dirisha dogo la Januari mwaka huu, Brom iliwasijili, Robert Snodgrass, Andy Lonergan, Mbaye Diagne na Okay Yokuslu.

Akizungumzia kilichotokea kwa Musa, Kocha wa West Brom, Sam Allardyce amesema, "tulinunua wachezaji wanne, hatukuwa na bajeti ya kukamilisha usajili wake.

"Ni aibu kwamba Musa hakuja mapema kutokana na taratibu za corona, pengine angekuwa miongoni mwa wachezaji wanne tuliowanunua, lakini alikuwa wa tano na hatukuweza kufanya hivyo."



# DON A SOKA
## MAGA A ULAYA




# BAYERN YAMSAJILI RASMI UPAMECANO

### Ni baada ya vigogo hao wa Bundesliga kukubali kulipa dau lililoko kwenye mkataba...

**MUNICH,** Ujerumani

DAYOT Upamecano atajiunga na Bayern Munich kutoka RB Leipzig msimu ujao akiwa tayari amekubali mkataba wa miaka mitano, Mkurugenzi wa Michezo wa mabingwa hao, Hasan Salihamidzic amethibitisha.

**Upamecano kwa muda mrefu amekuwa akihusishwa na mpango wa kuondoka Leipzig baada ya kuchomoza kama mmoja wa walinzi bora kabisa barani Ulaya kwa sasa.**

Katika wiki za hivi karibuni amekuwa akitajwa zaidi, huku klabu za Liverpool, Chelsea na Bayern zote zilionyesha nia ya kumwinda.

Wakala wa Upamecano hivi karibuni alithibitisha mlinzi huyo ana kipengele cha euro milioni 42.5 kwenye mkataba wake ambacho klabu yoyote itakayotaka kumsajili lazima ikilipe, akiwa amesaini mwaka jana.

Na kwa kiasi hicho Bayern inajiandaa kulipa, huku Salihamidzic akibainisha kwamba majadiliano yao yalifikia mwafaka wiki iliyopita.

Alipoulizwa na Sport Bild kama anaweza kuthibitisha kuhusu uhamisho huo, Salihamidzic alisema: "Naweza kufanya hivyo, na tuna furaha kubwa kuhusu hilo hapa FC Bayern.

"Tulikuwa na nia nzuri sana, tumefanya majadilinao ya kitaalamu na Dayot na mshauri wake, Volker Struth kwa miezi kadhaa.

"Tulijua kwamba tuna ushindani mgumu. Upamecano ni mchezaji kijana, mwenye miaka 22, ambaye ubora wake ameshauthibitisha.

"Mara zote nilishawishika kwamba tumekuja na wazo zuri sana. Tunamwangalia kwa dira yetu na muda wake wa kucheza hapa FC Bayern.

"Kwa wiki iliyopita mjini Doha, nilizungumza na kila mmoja aliyehusika. Mwisho wa siku baada ya machakato mrefu, wachezaji na uongozi tukashawishika kwamba, FC Bayern ilikuwa sehemu bora zaidi kwake na atakuwa 'patina' mzuri wa klabu hii."

Ilibainisha kwamba, Bayern walikubali kulipa fedha iliyopo kwenye kipengele cha mkataba na Upamecano kupewa miaka mitano, kitu ambacho alikubali: "Ni kweli. Dayot Upamecano ataichezea FC Bayern kwa miaka mitano ijayo."

## ZISIKUPITE

### SANCHO NJIA PANDA

WINGA wa Borussia Dortmund na Timu ya Taifa ya England, Jadon Sancho (20), amesema pengine atacheza klabu nyingine msimu ujao, lakini kuna matumaini finyu juu ya miamba hao wa Ujerumani kumuuza kwa pauni milioni 100 ambazo walikuwa wakitaka Manchester United wazitoe miezi sita iliyopita. ***(Eurosport)***

### WIJNALDUM KUONDOKA

LIVERPOOL inajiandaa kuondoka kwa kiungo wake, Georginio Wijnaldum mwenye umri wa miaka 30, na wanataka kumsajili kiungo wa Borussia Monchengladbach, Florian Neuhaus (23), kama mrithi wake. ***(Kicker)***

### KLOPP AMTAKA DE PAUL

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp, anatarajiwa kujaribu kumsajili mshambuliaji wa Udinese na raia wa Argentina, Rodrigo de Paul, kwa dau la pauni milioni 30. ***(Sun)***

### ARSENAL YAJIPANGA

ARSENAL wanaamini wanaweza kumshawishi mshambuliaji wao kinda, Folarin Balogun (19), kusaini mkataba mpya. Mkataba wa chipukizi huyo wa England unafikia ukomo mwishoni mwa msinu huu na tayari kuna klabu kadhaa barani Ulaya zinamnyatia. ***(London Evening Standard)***

### BALOGUN AGOMBEWA

KLABU za Ujerumani, Bayer Leverkusen na Stuttgart pamoja na Rennes ya Ufaransa ni baadhi ya timu zinazowania saini ya mshambuliaji wa Arsenal, Folarin Balogun ambaye ana umri wa miaka 19. ***(Mirror)***

### GREALISH KAMA MESSI

GOLIKIPA wa Aston, Villa Emiliano Martinez amemlinganisha kiungo Jack Grealish mwenye umri wa miaka 25 sawa na mshambuliaji wa Barcelona, Lionel Messi. ***(Talksport)***

### VIEIRA APIGIWA PANDE

KLABU ya Bournemouth ambayo haina kocha kwa sasa, imeshauriwa na mchezaji nguli wa zamani wa Arsenal, Martin Keown kumchukua kiungo wa zamani wa washikabunduki hao, Patrick Vieira (44), kuwa kocha wao mpya. ***(Talksport)***

### GIBBS LULU MAREKANI

KLABU za New York Red Bulls na DC United zote za Marekani zinapima mizani kabla ya kujitosa katika mbio za kumsajili beki wa West Bromwich, Albion Kieran Gibbs, ambaye ana umri wa miaka 31 na anawaniwa na Inter Miami ya Marekani. ***(ESPN)***

### COSTA ANUKIA PALMEIRAS

MSHAMBULIAJI wa Hispania, Diego Costa mwenye umri wa miaka 32, ambaye aliondoka Atletico Madrid Disemba, mwaka jana, yupo katika mazungumzo ya kujiunga na Palmeiras ya nchini Brazil ambayo alikuwa akiishabikia tangu utotoni. ***(Sky Sports)***

## Hitimana 'aona mwanga' Mtibwa

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Mtibwa Sugar, Thiery Hitimana, amesema kikosi chake kina mabadiliko makubwa na hali hiyo inampa matumaini ya kufanya vizuri katika mechi za mzunguko wa pili Ligi Kuu Tanzania Bara zinazoendelea.

Hitimana alisema mabadiliko hayo ni katika safu ya ulinzi, kiungo pamoja na ushambuliaji ambao awali walikosa umakini kwa kupoteza nafasi wanazozitengeneza.

Alisema baada ya kucheza mechi ya kirafiki dhidi ya Dodoma jiji FC, kwa kuibuka na ushindi wa mabao 2-1, ameona 'mwanga' kwa kubaini upungufu na kuyafanyia kazi kabla ya kucheza mechi ya ligi.

"Mechi hiyo ya kirafiki imenisaidia sana na sasa nafanyia kazi udhaifu ambao nimebaini katika mchezo huo kuelekea mchezo wetu dhidi ya Ihefu FC ambayo tutacheza nao hapa nyumbani.

Kocha huyo alisema mechi hiyo haitakuwa rahisi kwa sababu tunahitaji kupata matokeo chanya ili kujiimarisha katika msimamo wa ligi kama ambavyo wapinzani wao Ihefu watakavyoingia na malengo ya kuchukua pointi tatu.

## Jang'ombe Boys, KVZ majaribuni

**Na Hawa Abdallah,** Zanzibar

MASHINDANO ya Kombe la FA Zanzibar yanatarajiwa kuanza rasmi kesho kwa JKU inayoshiriki Ligi Kuu Zanzibar kuwakaribisha Super Tiger ya Ligi Daraja la Pili Mkoa wa Kusini kwenye Uwanja wa Wimbi visiwania hapa.

Mechi nyingine ya mashindano hayo itakayochezwa kesho ni kati ya KVZ dhidi ya Jang'ombe Boys ambayo inashiriki Ligi Daraja la Kwanza Kanda ya Unguja.

Mkurugenzi wa Kamati ya Mashindano ya Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), Ali Mohammed Ameir, alisema tayari kamati imetoa ratiba ya awali ya michuano hiyo huku mwendelezo wake utafuata baada ya Bodi ya Ligi kutoa ratiba ya mechi za mzunguko wa pili wa Ligi Kuu visiwani hapa.

Ameir alisema maandalizi ya michuano hiyo yamekamilika kwa upande wa timu za Unguja na kamati inaendelea kuhakikisha Kanda ya Pemba pia inakamilisha maandalizi yake ili michuano hiyo ichezwe kwa kufuata kalenda ya mashindano iliyopo.

# BIASHARA YAIPONGEZA SIMBA, YAITAHADHARISHA

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Biashara United, Mkenya Francis Baraza, amesema kwa sasa Simba imejiwekea heshima kubwa katika soka la Afrika baada ya kufanikiwa kupata pointi tatu muhimu katika mchezo wa kwanza wa ugenini katika hatua ya makundi ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

**Simba inayonolewa na Mfaransa Didier Gomes ilifanikiwa kuvuna pointi tatu muhimu baada ya kupata ushindi wa bao 1-0 dhidi ya wenyeji AS Vita Clu katika mechi ya Kundi A iliyofanyika juzi jijini Kinshasa, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Chris Mugalu akifunga goli hilo pekee kwa penalti dakika 60 ya mchezo huo.**

Kikosi cha mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara kinatarajia kurejea nchini keshokutwa na itasafiri kuelekea mkoani Mara kuwafuata Biashara United katika mechi yake ya ligi itakayochezwa Februari 18, mwaka huu kwenye Uwanja wa Karume mjini Musoma.

Akizungumza na gazeti hili jana, Baraza alisema amefanikiwa kuufatilia mchezo huo kwa umakini na kuona jinsi Simba ilivyocheza kwa nidhamu ya hali ya juu na uwezo mkubwa wa kutafuta matokeo na kufanikiwa kuyapata.

Baraza alisema kitendo walichokifanya Simba katika mchezo huo wa kimataifa kimewapandisha 'daraja' na kuwaamsha wapinzani wao kujipanga zaidi wanapokutana na wawakilishi hao wa Tanzania.

"Haya matokeo na mpira ambao wamecheza Simba, nina imani kuna kitu wamekijenga kwa Afrika, ukiangalia katika mchezo dhidi ya AS Vita, Kocha Ibenge (Jean Florent), alitumia mshambuliaji mmoja hii ilionyesha jinsi gani ambavyo waliingia kwa kuwaogopa wapinzani wao, kwa kutumia mshambuliaji mmoja," alisema Baraza.

Kocha huyo alisema Simba kupata pointi tatu ugenini ni jambo 'kubwa sana' na imejiweka katika moja ya timu zinazojadiliwa na kutengeneza kitu kwa wapinzani ambao wanakuja kukutana nao hivi karibuni kwenye Uwanja wa Benjamina Mkapa.

"Kwa upande wangu nimejipanga , tunatarajia kukutana na Simba baada ya kurejea kutoka DRC wanakuja nyumbani (Musoma), tunacheza nao, kwa jinsi nilivyowaona tunaendelea kujipanga zaidi, kuhakikisha tunapambana nao kupata matokeo chanya," alisema Baraza.

Aliongeza kila mechi huwa na mipango yake hivyo anaamini mbinu alizowapatia wachezaji wake zitasaidia kusaka matokeo chanya katika mchezo huo.

"Tunajua siku zote hakuna mechi rahisi, tutaikabili Simba kulingana na watakavyokuwa siku hiyo, hakuna mechi ndogo au kubwa katika dunia ya sasa, tutajituma na tunaamini lolote linaweza kutokea tutakavyokutana," Baraza alisema.

Yanga yenye pointi 44 (kabla ya mechi yake ya jana), ndio vinara wa ligi hiyo wakifuatiwa na Simba yenye pointi 39, Azam FC yenye pointi 33 na Biashara United yenye pointi 29 iko katika nafasi ya nne.



Nahodha wa Simba, Mohamed Hussein 'Zimbwe Jr' (kulia), akijiandaa kuwatoka wachezaji wa AS Vita katika mechi ya Kundi A ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika iliyochezwa jijini Kinshasa, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), juzi usiku. Simba ilishinda bao 1-0. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# *CAF yafuta mchezo wa Namungo, De Agosto*

**Na Saada Akida**

SHIRIKISHO la Soka Afrika (CAF), limetangaza kuufuta mchezo wa hatua ya mtoano wa Kombe la Shirikisho Afrika kati ya wenyeji C.D de Agosto ya Angola dhidi ya Namungo FC kutoka Tanzania, imeelezwa.

Mechi hiyo kati ya De Agosto na Namungo ilitarajiwa kuchezwa leo nchini humo.

CAF imefikia uamuzi huo kutokana na kuwapo kwa sintofahamu baada ya msafara wa Namungo kuwekwa karantini na wenyeji wao huku wakidaiwa wachezaji wao watatu na kiongozi mmoja ana ugonjwa wa corona.

"Kutokana na kadhia hiyo, CAF imesema suala kuhusu mechi hiyo litafikishwa katika kamati husika kwa ajili ya uamuzi," ilisema sehemu ya taarifa ya CAF.

Mapema jana Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa alisema serikali kutumia maofisa wake wa Wizara ya Mambo ya Nje, kikosi cha timu hiyo kitakamilisha majukumu yake na kurejea nchini salama.

"Tutatumia maofisa wetu wa Wizara ya Mambo ya Nje kumaliza matatizo yaliyowakuta, tunajua hizo zi siasa za michezo," alisema Majaliwa.

Naye Mwenyekiti wa Namungo, Hassan Zidadu, ambaye aliambatana na timu hiyo aliliambia gazeti hili kikosi chao kilizuiliwa kwenye uwanja wa ndege baada ya kuelezwa wachezaji watatu na kiongozi mmoja wamebainika wana virusi vya corona.

# Michezo

Jumapili Februari 14, 2021

Nipashe




Bayern yamsajili rasmi Upamecano

HABARI UK 22

# SIMBA YATETEMESHA AFRIKA

●●●Ni baada ya kuweka rekodi ya kupata ushindi ugenini, pongezi zamiminika....



Kiungo wa kimataifa wa Simba, Clatous Chama (kulia), akijiandaa kumtoka kiungo mkabaji wa AS Vita, Papy Tshishimbi (kushoto), katika mechi ya Kundi A ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika iliyochezwa jijini Kinshasa, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), juzi usiku. Simba ilishinda bao 1-0. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

**Adam Fungamwango na Augusta Njoji, DODOMA**

USHINDI wa bao 1-0 ilioupata Simba ikiwa ugenini nchini Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC), dhidi ya AS Vita katika mechi ya Kundi A ya Ligi ya Mabingwa Afrika umeijengea heshima timu hiyo na kuwapa furaha wadau mbalimbali wa soka hapa nchini.

Kwa muda mrefu AS Vita imekuwa ikizionea timu za Ukanda wa Afrika Mashariki kwa kuzipa vichapo kila inapokuwa kwenye uwanja wake wa nyumbani, lakini juzi kibao kiliwageukia Wakongomani hao.

Straika mzaliwa wa nchi hiyo, Chriss Mugalu, aliipatia Simba bao pekee katika mchezo huo kwa penalti dakika ya 61 kufuatia shuti la Luis Miquissone kumgonga mkononi, Qusmane Quttara na mwamuzi kuamuru tuta lipigwe.

Kocha Mkuu wa Simba, Didier Gomes, amesema amefurahishwa na ushindi huo na kuongeza ni mwanzo mzuri wa kuelekea kufanya vyema kwenye kundi hilo.

"Tunafuraha na tumeridhika na ushindi tulioupata kwa sababu tumecheza vizuri na tumepata matokeo mazuri kwa timu yetu ambayo yatatusaidia baadaye kwenye hatua hii ya makundi," alisema Gomes.

Kocha huyo alisema amefurahishwa na jinsi wachezaji wake walivyopambana na kucheza kwa kufuata maelekezo aliyowapa kwa sababu kila mmoja alifahamu AS Vita si timu ya mchezo.

"Unajua michuano hii ni lazima ucheze kwa mbinu zaidi. Niliwaambia vijana wangu kutowapa nafasi wapinzani ya kusogea hatua nyingi zaidi wakiwa na mpira. Nikawaelekeza jinsi ya kucheza wakiwa na mpira na wakiwa hawana, AS Vita ni timu inayojua kufanya mashambulizi ya kushtukiza, hasa mnapojisahau na kupanda mbele," alisema Didier.

Nahodha wa timu hiyo, Mohamed Hussein 'Zimbwe Jr' , alisema wametimiza kile ambacho walitumwa na Watanzania kwenda kukifanya na wametimiza, huku akishukuru mapokezi mazuri waliyoyapata nchini humo.

"Ni mara ya pili nawaona mkicheza hapa. Mwaka 2018 tulitoka tumenyong'onyea, lakini mechi hii mmecheza kwa kujiamini. Tangu mwanzo niliongea na nyinyi machoni niliona ushindi, na haikuwa na kubahatisha, mmeonyesha uwezo mkubwa sana na mmeipa heshima kubwa nchi yetu," Balozi wa Tanzania DRC, Luteni Jenerali Mstaafu, Paul Mella alisema.

Balozi huyo alisema mtu wa kwanza kumpigia simu baada ya mechi kumalizika alikuwa ni Spika wa Bunge, Job Ndugai akiwapongeza wachezaji, benchi la ufundi na viongozi kwa ushindi huo wa kihistoria.

**SHANGWE BUNGENI**

KAMA ilivyo ada, ushindi huo wa Wekundu wa Msimbazi umelitikisa bunge huku serikali ikitoa pongezi na kusema ni ushindi wa uchumi wa kati.

Hali hiyo ilijitokeza jana kwenye hotuba ya Waziri Mkuu Kassim Majaliwa na Waziri wa Katiba na Sheria, Dk. Mwigulu Nchemba.

Akitoa hotuba ya kuahirisha bunge jana, Waziri Mkuu alipongeza timu hiyo pamoja na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Simba, Barbara Gonzalez kwa ubunifu wa kushirikisha Wizara ya Maliasili na Utalii na hivyo kulipa heshima taifa kwa kulitangaza kupitia jezi yao yenye maneno 'Visit Tanzania'.

"Kwa mujibu wa maelezo yake, neno 'Visit Tanzania' linakadiriwa kutazamwa na wapenzi wa soka takriban milioni 500 kutoka sehemu mbalimbali duniani, kupitia vituo vya Televisheni vya Canal Algérie, BeIN Sports, Eurosport, ESPN, Arryadia, GTV ya Ghana, MENA beIN Sports na West Africa Canal na imeshuhudiwa kwenye mchezo wa jana (juzi),"alisema.

Akijibu hoja za wabunge waliochangia Mpango wa tatu wa maendeleo ya taifa wa miaka mitano, Waziri Mwigulu alisema "Tanzania hatukufanya maombi wala kulipia kuingia uchumi wa kati bali ni jambo lililozingatia vigezo...Wewe unayepinga kwanini? Unaona sifa kuitwa maskini? Tunaona hata timu ya Simba kushinda juzi ni uchumi wa kati maana viwango vyao vilikuwa vya uchumi wa kati."

Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Haji Manara, alisema kikosi cha timu hiyo kinarejea leo mchana lakini akiomba mashabiki wasijitokeze kuwapokea kwa sababu bado hawajamaliza kazi kwenye mashindano hayo.

## Yanga yashikwa

**Na Adam Fungamwango**

BAO la mkwaju wa penalti kwenye dakika tatu za nyongeza lililofungwa na straika wa zamani wa timu za Stand United, Simba na Mbao FC, Pastory Athanas, liliinyima ushindi Yanga kwa kulazimishwa sare ya goli 1-1 dhidi ya Mbeya City katika mechi ya Ligi Kuu Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya jana.

Wakati mashabiki wa Yanga walidhani wanaondoka na pointi tatu, mpira wa faulo uliopigwa kwenye lango la Yanga ulimgonga mikononi, Yassin Mustapha na mwamuzi kuamuru kuwa ni penalti, iliyowekwa wavuni kwa ustadi na Athanas aliyemuacha Metacha Mnata akiruka kushoto, mpira ukienda kulia.

Zilikuwa dakika nane za mwisho za kusisimua kwani ndizo zilizopatikana mabao yote mawili.

Dakika tano kabla ya pambano kumalizika, Yanga iliandika bao kupitia kwa Deus Kaseke, lililotokana na kujichanganya kwa mabeki wa Mbeya City na kumruhusu nyota huyo wa zamani wa wenyeji kufunga bao la utangulizi.

Kaseke ambaye jana alifikisha bao la tano msimu huu, aliudokoa mpira uliosereka wavuni, licha ya juhudi na Salum Chitembe kuuokoa, lakini tayari ulikuwa umevuka mstari wa goli.

Kwa matokeo hayo hayo, Yanga inaendelea kuongoza ikiwa na pointi 45 kwa mechi 19 ilizocheza, pointi saba juu ya Simba inayoshika nafasi ya pili kwa pointi 39 na mechi 17 ilizocheza huku Mbeya City yenye pointi 15 ipo kwenye nafasi ya 17.

9 770856 541002

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042